epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Januari 23, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581930

www.ippmed...

nipasheTZ nipasheTZ The Nip... ...al nipasheTZ nipashedigital

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com

AWAMU YA NNE



# CHADEMA ya zama za Lissu

- **Kura** 31 zamvusha, akataa kisasi, Mbowe amwachia haya
- **Vilikuwa** vita vya hoja, akaonesha umahiri kupangua, ataka Mnyika aendelee
- **Askari** binafsi ulinzi hadi msalani, FFU wabaki likizo
- **Mfumo** mpya viti maalum udiwani, ubunge, uenyekiti
- **Swahiba** wa Mbowe, miongo miwili kutoka gerezani... *Ukurasa 2, 3, 4 na 18*



Said Mzee Said



John Heche



UKURASA WA 21

## SALAH AWEKA HISTORIA LIVER

## Mgombea Dk. Mwinyi apokewa Zanzibar kwa mbwembwe

UKURASA 5



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali baada ya kuwaapisha majaji wa Mahakama ya Rufani, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia ampa jukumu Mganga Mkuu mpya magonjwa mlipuko

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA: KUCHEZA BILA MASHABIKI ILITUUMIZA UK.24 **KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA




Mwenyekiti Mpya wa Chadema Taifa, Tundu Lissu, akizungumza na wajumbe wakati akiwashukuru baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo, katika mkutano mkuu wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Bara, John Heche. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ni zama za kina Lissu CHADEMA

**Na Restuta James**

BAADA ya timu zao za kampeni kutambiana kwa mwezi mmoja, hatimaye Tundu Lissu amekuwa Mwenyekiti wa nne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akimshinda Freeman Mbowe kwa tofauti ya kura 31.

Katika uchaguzi huo ulioanza juzi na kukamilika jana asubuhi kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, Lissu alitangazwa mshindi baada ya kupata kura 513 sawa na asilimia 51.5 dhidi ya Mbowe aliyepata kura 482 sawa na asilimia 48.3 huku mgombea mwingine Odero Charles akiambulia kura moja.

Akifunga Mkutano Mkuu wa chama hicho baada ya kutangazwa mshindi, Lissu alisema hatolipa kisasi kwa yeyote bali atahakikisha kila mmoja anapata haki.

“Tuna kazi ya kuwaambia wale waliofanyiwa kila aina ya vitimbi, walioenguliwa kwa njia za ajabu ajabu, tunahitaji kwenda kuwaambia tulifanya makosa, tunaomba msamaha sasa tuhakikishe kwamba haya mambo yaliyosababisha maumivu yote haya katika uchaguzi wetu hayajirudii tena. Si ya leo, na ya jana na juzi. Tutaenda huko tulikoanzia.

"Tutawarudisha wale waliokata tamaa, tutawapa tumaini jipya. Tutaombana msamaha, hatutalipizana visasi. Mimi ni mtu wa haki. Hatutalipiza kisasi, tutaponya wote walioumizwa," alisema.

"Na hili la juzi, hiyo chinjachinja ya wagombea nafasi za Kamati Kuu, hizi ambazo uchaguzi unafanywa Baraza Kuu, hayo maumivu tutaanza nayo. Wamekata rufani, tutazisikiliza kama zina haki, tutawarudisha," alisema.

Lissu pia alisema marekebisho ya katiba ya chama hicho yataweka ukomo kuwa awamu mbili pekee ili kiongozi aondoke madarakani kwa heshima.

Kuhusu nafasi za viti maalum, Lissu alisema uongozi wake utaweka utaratibu wa kikatiba na kikanuni kuhakikisha kila mwanamke ambaye ni mwanachama wa CHADEMA, anapata haki sawa ya kugombea kwenye kata, majimbo na viti maalum.

Kuhusu ushauri aliopewa na Mbowe kuponya majeraha ya mchakato wa uchaguzi, Lissu alisema hayajaanzia kwenye uchaguzi mkuu bali kwenye ngazi mbalimbali.

Alisema uongozi wake utafanya kazi ya kujenga upya chama hicho kwa kuwa baadhi ya wagombea walienguliwa kwa mizengwe na figisu.

Kuhusu fedha, Lissu alisema timu yake itatafuta fedha na kuzitumia kwa maslahi mapana ya chama hadi ngazi ya tawi.

Alisema kila ngazi ya uongozi itafanya kazi yake kwa uhuru, kinyume cha ilivyokuwa awali, maofisa wa makao makuu walikuwa wanahusika katika ngazi mbalimbali.

Lissu alisema kazi iliyoko mbele yao ni kudai mambo manne ambayo ni Katiba mpya, mifumo huru ya uchaguzi wenye tume huru na sheria bora za uchaguzi. Yasipopatikana hakutakuwa na uchaguzi.

Makamu wake, John Heche alisema watafanya kazi usiku na mchana, kukijenga na kukikilinda chama hicho, akisisitiza "...tafsiri ya uchaguzi huu ni kwamba mtu yeyote asiye na ubini wa jina kubwa anaweza kuwa kiongozi mkubwa. Tunamshukuru sana Mbowe kwa kukijenga chama hiki, na sisi tutakilinda kwa ajili ya watanzania."

Jana jioni, kikao cha kwanza cha Baraza Kuu la Chama chini ya Mwenyekiti mpya Lissu kiliitishwa kwa ajili ya kupata wajumbe wanane wa Kamati Kuu, lakini uchaguzi huo uliahirishwa kutokana na wagombea 19 kukata rufani kupinga kuenguliwa.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, uchaguzi wa wajumbe hao utafanyika baada ya Kamati Kuu kuketi na kutoa uamuzi wa rufani zilizokatwa.

# Samia ampa jukumu Mganga Mkuu kudhibiti magonjwa ya mlipuko

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemtaka Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Grace Magembe kudhibiti milipuko ya magonjwa inayoweza kusababisha nchi kuingia katika changamoto mbalimbali ikiwamo kuzuiwa kwa safari za kimataifa.

Alitoa agizo hilo jana Ikulu ya Chamwino, mkoani hapa, wakati wa hafla ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni.

Alisema nafasi ya Mganga Mkuu wa Serikali ni jukumu kubwa na anapaswa kwenda kushirikiana na timu yake kudhibiti milipo ya magonjwa nchini.

"Niwaombe viongozi mlioteuliwa na kuhamishwa vituo vyenu vya kazi hivi karibuni mnakwenda kutimiza majukumu yenu hususan nafazi ya Mganga Mkuu wa Serikali ni nafasi kubwa sana ambayo inahitaji umakini mkubwa sana.

"Sasa nikuagize Mganga Mkuu wa Serikali kuhakikisha unashirikiana na timu yako kwenda kuzuia milipuko ya magonjwa ambayo inayohofiwa kuifanya nchi yetu kutajwa na mataifa mengine kuwa ni sehemu ya milipuko ya magonjwa na kusababisha nchi yetu kufungiwa safari za nje," alisisitiza Rais Samia.

Vilevile, aliwaagiza Majaji wa Mahakama ya Rufani aliowaapisha kwenda kuutumia vizuri uhuru wa muhimili huo kwa kutenda haki na sio vinginevyo.

"Uhuru wa muhimili wa mahakama uendelee kutumika vizuri kwa ajili ya kutoa haki kwa Watanzania wote na nyie mkawe sehemu ya mabadiliko katika maeneo yenu mliochaguliwa," alisema.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema hatua ya Rais Samia kufanya uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani kutasaidia kupunguza changamoto mbalimbali ikiwamo mlundikano wa mashauri pamoja na wafungwa na mahabusu.

"Mheshimiwa Rais uteuzi huu wa Majaji wa Mahakama ya Rufani umefanya idadi yao kuongezeka kutoka 35 hadi 39 hali hii inakwenda kusaidia kupunguza mrundikano wa mashauri pamoja na wafungwa na mahabusu.

"Mwezi Novemba, mwaka jana, nilitembelewa na Kamishna Jenerali wa Magereza akaniambia kuwa haya maboresho yanayofanywa na serikali ikiwamo ongezeko la majaji imewasaidia sana kupunguza sana mrundikano wa wafungwa na mahabusu," alisema.

Alisema, kwa mujibu wa Kamishna wa Magereza inao uwezo wa kuhifadhi wafungwa 29,000, lakini kutokana na uwekezaji katika muhimili wa Mahakama hivi sasa kuna nafasi ya wafungwa 2,000 ambayo ipo wazi.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Grace Magembe, aliteuliwa hivi karibuni kushika nafasi ya Profesa Tumaini Nagu, ambaye uteuzi wake ulitenguliwa na Rais Samia.

Kabla ya kuteuliwa, Dk. Magembe alikuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.


**TANGAZO KUPOTEA NYARAKA UMILIKI KIWANJA**

**LETECIA MASAMAGA LIMA**

anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki kiwanja namba 934 kitalu "PP" kilichopo Ndembezi Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/SHI/SHI/414/2025.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MUNA ABDALLAH TALIB**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE JINA LA JOSEPH ABEL FUNGO YENYE NAMBA YA USAJILI **T 896 BKA** MISTUBISH COLT.

ENGINE NO **4G19CY6633.**

CHASSES S NO **Z25A0037562.**

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/ARU/ARU/ 2226/2025.**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED I SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH** of **DAR ES SALAAM DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name of **SHADIA ABDULAZIZ ABDALAH** as it can be seen my National Identity Card **(NIDA)** also the name **SHADYA ABDULAZIZ ABDALA** as it can be seen my standard seven Certificate **FOR THE REASON THAT** during the registration of the identity card and in my Certificate there was typing error on writing my names **SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH** they wrote **SHADIA ABDULAZIZ ABDALAH** and **SHADYA ABDLAZIZ ABDALA** and that position and from now I want to use and to be known as **SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH** and as from the date of this deed poll and in substitution of my name and use the name **SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH** as it appears in my Birth Certificate and in my Academic Certificate.

For the purpose of evidence such determination, I hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action suits and proceeding as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH** as my name in lieu of and in substitution for my former name of **SHADIA ABDULAZIZ ABDALAH** and **SHADYA ABDULAZIZ ABDALA. AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH.**

**IN WITNESS WHEREOF I** have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old name of **SHADIA ABDULAZIZ ABDALLAH** and **SHADYA ABDULAZIZ ABDALA** by my new name of **SHADYA ABDULAZIZ ABDALLAH.**

SIGNED and DELIVERED by the said SHADYA ABDULAZIZ ABDALAH who is known to me personally/identified to me by ........................ the latter being known to me personally in my presence this 13 day of Jan 2025

DEPONENT

BEFORE ME

Signature:

Postal address:

Qualification: ADVOCATE AND COMMISSIONER FOR OATH

**TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA EXCAVATOR**

**SULTAN SIMON NZOYA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA EXCAVATOR AINA YA EXCAVATOR - **CAT 320** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 641 DTT**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI

**PHQ/SHI//KAH/456/2025.**

# Undani uchaguzi wa CHADEMA

Na Elizabeth Zaya

- Lissu akosoa hoja kutobadili jenerali katikati ya vita
- Zitto ampongeza Mbowe kwa ukomavu wa kisiasa




Ulinzi ukiwa umeimarishwa kwa Mwenyekiti Mpya wa Chadema Taifa, Tundu Lissu na Makamu Mwenyekiti Bara, John Heche, wakati wa mkutano huo, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

HISTORIA imeandikwa katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kikipata mwenyekiti mpya baada ya miaka takribani 20 ya uongozi wa Freeman Mbowe.

Tundu Lissu anakuwa mwenyekiti wa nne katika historia ya CHADEMA baada ya kuwashinda Mbowe na Odero Charles katika uchaguzi uliofanywa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama usiku wa kuamkia jana na matokeo yake kutangazwa asubuhi ya jana.

Mchuano wa uchaguzi huo ulikuwa mkali, hasa kwa wagombea wawili; Lissu na Mbowe, wote waliwahi kuwa wabunge wa Singida Mashiriki na Hai. Mbali na ubunge na kushika nafasi mbalimbali ndani ya CHADEMA, Lissu pia aliwahi kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).

Uchaguzi ndani ya CHADEMA uliibua hisia na mambo mengi kwenye demokrasia ya Tanzania kwa zaidi ya mwezi mmoja tangu kuanza kampeni zao zilizosheheni minyukano baina ya wafuasi wa pande hizo mbili.

Uchaguzi huo uliohusisha nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti Bara na Tanzania Zanzibar, ulianza juzi Januari 21 na kukesha mpaka jana asubuhi, mshindi alipotangazwa.

Mapema juzi asubuhi, kwenye viwanja vya Mlimani City ulikofanyika uchaguzi huo, wajumbe pamoja wafuasi na wapambe wengine walifika wakiwa wanaimba nyimbo na kushangilia wakitaja jina la mgombea wanayemuunga mkono.

Hawakuishia kwenye nyimbo tu, wapo waliofikia hatua ya kushikana mashati wakati wa kutambiana wakiwa kwenye maeneo ya biashara za chakula na starehe ya karibu na Ukumbi wa Mlimani City ulikokuwa unafanyika uchaguzi huo.

Kwenye viwanja hivyo, nje ya ukumbi wa mkutano huo, mwandishi wa habari hii alishuhudia watu wengi, baadhi wakiwa wameketi kwa makundi wakifuatilia uchaguzi huo. Nyimbo za kejeli nazo zilikuwa sehemu ya uchaguzi huo.

Ndani ya ukumbi, chama hicho kiliweka walinzi maalum kutoka kampuni ya ulinzi kuzuia mtu yeyote asiyehusika kuingia ndani na katika kipindi chote cha upigaji kura, hakukuwa na mtu aliyeruhusiwa kutoka ukumbini.

Ulinzi uliimarisha hadi msalani, walinzi na wafuatiliaji maalum wa uchaguzi huo waliweka viti na kuketi pembeni ya milango ya kuingilia msalani na hawakuruhusu majadiliano yoyote kwa waliokwenda huko.

### WALIVYONADI SERA

Moja ya hatua zilizoteka hisia za wajumbe katika uchaguzi huo ni namna wagombea walivyonadi sera zao, hata maswali yaliyoulizwa na kujibiwa.

Katika hatua hiyo, wajumbe walizuiwa kushangilia, kuzomea au kucheka, lakini wakati mwingine zuio hilo lilishindikana kutekelezwa, yote hayo yaliyopigwa marufuku, yakafanyika.

Wakati akiomba kura, Mbowe alitoa tahadhari kwa wajumbe kwamba wasibadili jenerali katikati ya vita. Alisisitiza kubadili jenerali katikati ya vita ni hatari kwa ustawi wa chama hicho.

Odero kwa upande wake, aliwaomba wajumbe wamchagüe ili awapatanishe Mbowe na Lissu na timu zao kwa kuwa minyukano imesababisha mafarakano ndani ya CHADEMA.

Naye Lissu alitumia dakika zake tano za kuomba kura, kukosoa hoja ya Mbowe ya "kutokimbilia kubadili jenerali katikati ya vita", akikumbusha madhila ambayo chama hicho kimepitia katika uchaguzi wa mwaka 2019, 2020 na 2024.

Lissu ambaye ni mtaalamu wa sheria, alisema kuwa mwaka 2019, CHADEMA haikushinda hata mtaa mmoja katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; ikaambulia mbunge mmoja wa jimbo (kuchaguliwa na wananchi) katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na miezi miwili iliyopita imeambulia asilimia 0.8 ya mitaa na vijiji kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, lakini "jenerali yupo na hajafanya lolote kunusuru chama chake".

Ni kauli ambayo iliwafanya wajumbe kushindwa kuficha hisia zao, baadhi wakicheka, wengine wakimshangilia Lissu na wengine wakilaumu wasimamizi wa uchaguzi kwa kufumbia macho 'mashambulizi' ya Lissu kwa Mbowe.

Lissu alihitimisha hoja yake kwa kuwapa tahadhari wajumbe kwamba kwa kuzingatia mifano hiyo, walipaswa kuamua wamwongeze muda Mbowe aongoze kwa miaka 26 waendelee na madhila yaliyopo au wafanye mabadiliko kwa kumpa kura zao.

Kabla ya kupiga kura, kulifanyika uhakiki mkali wa wajumbe na kwa kipindi chote cha uchaguzi, wasimamizi walihakikisha unakuwa wazi, wajumbe wakiitwa kwa majina (wasiozidi sita) kwenda kupiga kura kwa kupeana nafasi na ilitolewa fursa kwa yeyote mwenye dukuduku au kuwa na taarifa yenye shaka, alipewa nafasi kueleza shaka yake na utatuzi wa utata kuhusu mjumbe husika ulifanyika hadharani.

Ni hatua iliyowezesha kubainika kuwapo wajumbe wachache ambao kikatiba hawakutakiwa kupiga kura hiyo au kutoka nje wakati wa shughuli hiyo inaendelea. Ilitolewa taarifa na wakaondolewa ukumbini.

Baadhi ya wajumbe wa uchaguzi huo, walipongeza namna utaratibu wa uchaguzi mwaka huu ulivyopangiliwa hususani katika eneo la kuufanya uwe wazi na kushuhudiwa na kila mtu aliyekuwa ndani na nje ya ukumbi.

### UCHAGUZI WARUDIWA

Uchaguzi katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar ulirudiwa baada ya wagombea wote wanne waliokuwa wakigombania nafasi hiyo kushindwa kufikisha asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa.

Kutokana na uchaguzi huo kurudiwa, utangazaji matokeo yote haukufanyika mpaka pale ulipokamilika uchaguzi wote. Hata hivyo, wafuasi wa Lissu waliokuwa ndani ya ukumbi na nje, tayari walikuwa wamepata taarifa za matokeo. Hawakusubiri tangazo rasmi, walishangilia ushindi muda huo huo, hata ikamlazimu Mbowe naye kukosa uvumilivu, akatumia kurasa zake za mitandao ya kijamii kuwapongeza Lissu na John Heche kwa kuchaguliwa kuongoza chama hicho.

"Nimepokea kwa mikono miwili uamuzi wa uchaguzi wa Mkutano Mkuu wa chama chetu cha CHADEMA uliohitimishwa leo (jana) asubuhi 22 Januari, 2025. Ninampongeza Mhe. Tundu Lissu na wenzake kwa kuaminiwa kutwikwa jukumu la uongozi wa chama. Ninawatakia kila la kheri katika kukipeleka mbele chama chetu," aliandika Mbowe.

Wagombea wawili ambao uchaguzi ulirudiwa kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Tanzania Zanzibar, ni Said Mzee Said na Said Issa Mohamed ambao walipata kura zaidi ya wenzao wengine wawili.

Mbali na Mbowe, Mwenyekiti Kanda ya Victoria aliyekuwa anagombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti, Ezekia Wenje pia alikubali matokeo na kuwapongeza Lissu na Heche kwa ushindi.

"Our people have spoken: Ninakupongeza sana Mhe TL (Lissu) na ndugu yangu Heche kwa ushindi, tutawapa ushirikiano pamoja na check and balance. Kwa walioniunga mkono pamoja na campaign team yangu, Mungu awabariki sana. To Freeman Mbowe you are the icon of our democracy," aliandika Wenje.

### WADAU WALONGA

Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, alimpongeza Lissu kwa ushindi na kumwahidi ushirikiano wa dhati katika harakati za kuimarisha demokrasia nchini.

Kupitia chapisho lake katika mtandao wa X, Dorothy, aliandika: "Ninakupongeza Ndugu Tundu Lissu kwa kushinda uchaguzi na kuwa Mwenyekiti wa chama chako cha CHADEMA. Kuchaguliwa kwako kunakufanya pia uwe Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD). Nikiwa Makamu wako huko, ninakukaribisha sana katika uongozi wa TCD.

"Nikiwa Kiongozi wa ACT Wazalendo ninakuhakikishia ushirikiano wa dhati katika kupigania demokrasia ya nchi yetu. Pia ninampongeza Mbowe kwa kukamilisha muda wake wa uongozi na kuonesha mfano wa ukomavu wa kisiasa."

Kiongozi mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, alimkaribisha Mbowe katika maisha mapya ya kustaafu huku akimpongeza kwa mchango wake aliotoa kwenye siasa za mageuzi nchini.

"Ninakukaribisha Mwenyekiti mstaafu Mbowe katika ustaafu na kukuhakikishia kuwa kuna mengi ya kufanya nje ya siasa za uongozi katika kazi kubwa iliyo mbele yetu ya kujenga na kustawisha demokrasia ya nchi yetu ambayo inatuhitaji wanamageuzi wote walio ndani na nje ya uongozi," aliandika Zitto.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@ guardian.co.tz***

# Mbowe aaga CHADEMA akiacha mambo mawili mezani kwa Lissu

**Na Restuta James**


ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameaga na kuwaomba viongozi wapya wa chama hicho kufanya mambo mawili, ikiwa ni pamoja na kutibu majeraha yaliyotokana na uchaguzi.

Amesema amefia kwenye demokrasia aliyoijenga, akisisitiza kuwa kushindwa kwake uchaguzi ni jambo analojivunia.

Wasimamizi wa uchaguzi wa viongozi wakuu wa CHADEMA uliofanywa na Mkutano Mkuu wa Chama katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, walimtangaza Tundu Lissu kuwa mshindi wa nafasi ya uenyekiti kwa kupata kura 513, akifuatiwa na Mbowe (482) na Odero Charles (1).

Akitoa salamu za kuwaaga wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CHADEMA baada ya Lissu (Mwenyekiti Taifa) na John Heche (Mwenyekiti Bara) kuibuka kidedea kwenye uchaguzi uliomalizika jana, Mbowe alisema moja ya mambo anayojivunia ni kujenga chama kinachoheshimu demokrasia na kinachoweza kufanya uchaguzi wake kwa uwazi, huru na haki mbele ya vyombo vya habari na dunia ikashuhudia.

"Ninamshukuru Mungu kwa kumaliza mkutano wote tukiwa salama salimini. Ninamshukuru Mungu kwa namna alivyoniwezesha kipindi changu kujenga chama chenye heshima, hadhi, maono, kilichojaa matumaini ya watu wote wanaoitamani kesho iliyo bora zaidi," alisema.



Mbowe alisema kuwa wakati wa kampeni kulikuwa na minyukano mikubwa, kiasi cha baadhi ya wanachama kumwambia atoke ili asiaibike, lakini alikataa na kuamua kubakia hadi mwisho kwa lengo la kuandika historia nzuri ya demokrasia ndani ya chama hicho.

"Nilisema nitafia kwenye demokrasia. Ninashukuru demokrasia niliyoijenga imesema. Tutahitaji demokrasia iendelee kusema kwa wengine wengi katika chama hiki na hata wengine wajifunze kwetu.

"Ninashukuru tumeonesha demokrasia kwa vitendo, ninaondoka nikiwa na roho nyeupe sana, nikijivunia kazi niliyoifanya kwa zaidi ya miaka 30. Ninawatakia viongozi wote yaliyo mema," alisema.

Mbowe alisema ataendelea kusaidiana na wenzake ndani ya CHADEMA kujenga chama hicho japokuwa kwa sasa anakwenda kujikita katika biashara zake.

### MAMBO MAWILI

"Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu, ninapokukabidhi kijiti, ninakuachia mambo mawili; tumefanya uchaguzi huru, haki na wazi, lakini uchaguzi ni mchakato. Uchaguzi kuwa hivi, halipaswi kuwa tukio la siku moja. Ninarudia tena, kwa namna kampeni zilivyoendeshwa, zimetuachia nyufa nyingi. Ni lazima tukubali na turekebishe.

"Uchaguzi huu umeacha majeraha mengi, kakiponyeni chama chetu. Niliahidi ningeshinda, ningeunda tume ya ukweli na upatanishi, watu wakazungumze yaliyojiri kwenye mchakato, pale walipokosa adabu wakasameheane ili chama chetu kikawe imara zaidi. Ushauri wangu kwako mwenyekiti na timu yako, ninawaasa undeni tume, tibuni majeraha ili mjenge chama chetu," alisema.

Mbowe pia aliwaomba kuepuka kiburi cha ushindi na kuunda kamati hiyo mapema ili Lissu na timu yake wafanye kazi kwa amani na wana-CHADEMA wote.

Alisema amefurahi kuona namna uchaguzi huo ulivyoendeshwa kwa uwazi, haki na ukweli na kwamba ndiyo historia aliyotaka kuiandika.

"Niliahidi tutafanya uchaguzi wa kihistoria, wengine walidhani ninadanganya, lakini dunia imeona. Tumemaliza salama, tunamshukuru Mungu," alisema.

Jambo la pili alilotaka Lissu alizingatie ni kuheshimu Katiba ya CHADEMA na kuepuka hisia kwenye uongozi, pale panapohitaji marekebisho, wayafanye kwa kushirikiana na wanachama wengine.

"Wakati wote, kijengeni chama hiki. Pale ambapo mnafikiri kwenye katiba kuna upungufu, shirikisheni wengine, fuateni taratibu za kistaarabu na za kidemokrasia, rekebisheni katiba, jengeni taasisi.

"Wana-CHADEMA wenzangu, kakiendelezeni hiki chama pale tulipoishia sisi, ninawaomba wanachama wote, viongozi wote, wa makundi yote wasaidieni viongozi hawa, kwa sababu wanaongoza taasisi ambayo sote sisi ni wadau. Tushikamane ili chama hiki kikawe na heshima iliyo bora zaidi," alisema.

Mbowe alisema kushindwa kwake uchaguzi kumempa likizo ya lazima ya kwenda kuendeleza biashara zake, akisisitiza kuwa yeye na Lissu ni marafiki wa kifamilia na hata mke wake, Dk. Lilian Mbowe alipompigia simu baada ya matokeo, alimpa Lissu azungumze naye.

### TUNDU LISSU

Lissu kwa upande wake, alisema Mbowe ni mjumbe wa kudumu wa Kamati Kuu ya chama na kushindwa uchaguzi hakumwondoi CHADEMA.

Alisema uchaguzi umekuwa huru, bila figisu wala mizengwe na kwamba chini ya Mbowe, CHADEMA imeweka ubora wa dhahabu.

"Nimshukuru kipekee kabisa Mbowe. Tumefanya kitu ambacho hatujawahi kukifanya katika chama hiki tangu kianzishwe, uchaguzi ambao hatujawahi kuufanya.

"Jana kabla hata hatujafikia kupigakura, nilikuwa ninazungumza na mwenyekiti na kitu kimoja ambacho tulizungumza, tumeweka ubora wa dhahabu. Chama kingine chochote ndani ya nchi kama wanatuweza, wafikie hapa," alisema.

Lissu alisema kuwa kila mjumbe aliyekuwa na haki ya kupiga kura, alipata nafasi hiyo na kura hiyo iliheshimiwa.

"Umefanya kitendo cha kiungwana sana kukubali matokeo, umepata muda wa kutupongeza. Tumefanya uchaguzi wa wazi, haki, huru na wa kidemokrasia. Tumshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti (Mbowe) kwa sababu aliahidi hivyo," alisema.

Lissu alisema kuwa chini ya Mbowe, chama hicho kimepata mafanikio makubwa kutoka kuwa na wabunge watano hadi kuwa chama kikuu na kikubwa nchini.

Mwenyekiti wa Uchaguzi huo, Frank Mwakajoka, alimshukuru Mbowe kwa kukubali matokeo na kuendelea kubakia ukumbini kwa muda mrefu.

"Nikupongeze sana Lissu kwa kushinda. Hapa tumekuja kupeana majukumu. Hatujaja kushindana. Ninaamini bado tunahitajiana, tunamhitaji Mbowe ili kuhakikisha kazi ya kuongoza dola inafikiwa," alisema.

## Watoto 1,700 wabadilishwa kuwa na tabia njema

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATOTO zaidi ya 1,700 waliokuwa vituo vya polisi kwa makosa madogo badala ya kupelekwa mahabusu za magereza, wamechepushwa katika uangalizi wa jamii na kubadilika na kuwa wenye tabia njema.

Ofisa Ulinzi wa Watoto wa Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), nchini Joseph Matimbwi, alisema hayo mjini hapa wakati akitoa salamu za Mwakilishi wa Shirika hilo nchini katika ufunguzi wa mafunzo ya ulinzi na usalama wa mtoto kwa maofisa na askari wa mapokezi wa Jeshi la Magereza ambao wanasimamia watoto magerezani.

Matimbwi ambaye pia ni Mratibu wa Programu ya Community rehabilitation Project, alisema kuwa programu hiyo ilianza mwaka 2013 katika mikoa miwili ya Dar es Salaam na Mbeya na mwaka 2016 ikaenda katika baadhi ya mikoa mingine nchini.

Alisema programu hiyo inahusika na watoto ambao hawafikishwi gerezani na imewasaidia wengi ambao wametoka kwenye uhalifu na wamerudi kwenye jamii wakiwa wenye tabia njema.

"Kuanzishwa kwa programu hii katika baadhi ya mikoa imesaidia mamia ya watoto kuchepushwa na kurudishwa tena kwenye tabia nzuri, wengine wamerudishwa shuleni na kwa wazazi wao ambao wanaendelea na tabia njema," alisema Matimbwi.

Aidha, imewasaidia watoto wengi kutoka kwenye uhalifu na kurudi katika jamii na baadhi wamekuwa mafundi wazuri kwenye fani mbalimbali na kutumika kwa jamii.

Matimbwi alisema UNICEF ipo tayari kuendeleza ushirikiano na Jeshi la Magereza katika kuona utofauti wa mtoto utakaoweza kuneemesha ustawi wake zaidi ambao anauhitaji.

Naye Kamishna wa Magereza, Nicodemus Tenga (Divisheni ya Sheria na Uendeshaji), alisema Jeshi la Magereza linapokea mfungwa au mahabusu kwa amri halali ya vyombo ambavyo kihalali vimeruhusiwa na sheria, kanuni na taratibu za nchi kuwaleta watu gerezani.

Tenga alisema jeshi hilo halina mamlaka ya kumleta mtu gerezani, bali mamlaka yake ni kumpokea, kumhifadhi, kumlinda, kumpa huduma na kumrekebisha.

Aidha, Kamishna wa Magereza, Bertha Minde (Huduma za Urekebu), alisema mafunzo hayo ni ya muhimu kwao katika kuhakikisha watoto waliopo magerezani wanapata ulinzi na usalama unaohitajika.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**ALEXANDER TINYA NDIMUBENYA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4436-0032 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DENDEGO SECONDARY SCHOOL mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi **MOR/KIL/RB/668841/2020**

**TANGAZO KUPOTEA NYARAKA UMILIKI KIWANJA**

**COLLETA FRANCISCO LUKALA** msimamizi wa mirathi ya **SIMON SHALALI MASHALA**

Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 429A kitalu "DD"Lubaga Manispaa ya Shinyanga. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/SHI/418/2025.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 263 LA 2024**
**ELITE PRE PRESS LIMITED .........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **REBECCA JANE YOUNG**
- **MWISHO MWAMPAMBA .........MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**REBECCA JANE YOUNG NA MWISHO MWAMPAMBA –**

**POPOTE MLIPO**

**ELITE PRE PRESS LTD** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo KInondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 25/02/2025 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaarifiwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 8 Mwezi 01...2025.




**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**LUSONYO BUZINGO**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 138 AVR – TOYOTA CALDINA. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/TEM/12891/2025.**

## Dk. Mwinyi apokewa kwa shangwe Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** Zanzibar

RAIS wa Zanzibar ambaye ni mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana alipokewa kwa shangwe baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Dk. Mwinyi aliwasili kutoka Dodoma kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa CCM baada ya kuidhinishwa kuwa mgombea urais wa Zanzibar kwenye uchaguzi utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Maelfu ya watu na wana CCM walifika kiwanjani hapo na baada ya kuwasili, Dk. Mwinyi alipokewa kwa shangwe na nderemo zilizoambatana na burudani za ngoma asili ya Kibari iliyokuwa ikitumbuizwa hapo.

Baada ya kutoka uwanjani akiwa katika gari maalum la wazi, alipita katika barabara za Uwanja wa Ndege, Kiembesamaki, Migombani, Kilimani hadi Ofisi Kuu ya CCM, Kisiwandui. Huko alilakiwa na wananchi na wafuasi wa CCM waliojipanga barabarani huku akiongozwa na matembezi ya waendesha bodaboda na watembea kwa miguu.

Alipofika Kisiwandui alikwenda katika kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Kadume, na kufanya kisomo cha dua kisha kuzungumza na wazee wa chama katika ofisi hizo za CCM.

Mgombea huyo aliondoka katika ofisi za CCM Kisiwandui majira ya saa 10:00 jioni na kwenda katika viwanja vya Mapinduzi Square, Kisonge mjini Zanzibar.

Kwenye viwanja hivyo, kulikuwa na burudani mbalimbali za wasanii kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Katika mapokezi hayo baadhi ya huduma za kijamii zilisimama takriban kwa muda wa saa tatu, huku usafiri wa daladala katika maeneo ya mjini ukiwa wa shida kutokana na barabara kufungwa.



# Noti mpya rasmi Februari Mosi

**Na Mwandishi Wetu**

NOTI mpya za Tanzania zenye saini ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) za toleo la mwaka 2010, zitaingia kwenye mzunguko kuanzia Februari Mosi, mwaka huu.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema hayo jana wakati akimkabidhi Dk. Nchemba, noti kifani za Sh. 10000; 5,000; 2,000 na 1,000 katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Dar es Salaam kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazosimamia masuala ya fedha nchini.

"Mheshimiwa Waziri, ninayo furaha kukujulisha kuwa uchapaji upya wa noti kwa marejeo ya toleo la mwaka 2010 uimekamilika na tayari tumewajulisha wananchi kupitia taarifa niliyoitoa kupitia Gazeti la Serikali," alisema.

Tutuba alisema noti hizo zitatumika sambamba na noti zilizopo hivi sasa na zina mwonekano wa noti zinazotumika sasa zilizotolewa mwaka 2010, zikiwamo alama za usalama, ukubwa, rangi na mambo mengine, isipokuwa ina marekebisho kwenye saini ya Waziri wa Fedha, na Gavana wa BoT.

"Saini ya aliyekuwa Waziri wa Fedha ambaye hivi sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Isdor Mpango, imebadilishwa na kuwekwa saini yako Mheshimiwa Dk. Mwigulu Lameck Nchemba na saini ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania aliyestaafu, Prof. Florens Luoga, imebadilishwa na kuwekwa saini ya Gavana wa Benki Kuu wa sasa, Emmanuel Tutuba," aliongeza.

Akizungumza baada ya kupokea sampuli za noti hizo mpya, Dk. Nchemba alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu jambo hilo kufanyika na kumpongeza Gavana Tutuba kwa kusimamia mchakato wa uchapaji wa noti hizo kwa weledi na uadilifu mkubwa.

"Mpaka kufikia hatua hii ni heshima kubwa kwa taifa letu na inaendeleza heshima ya wataalam wetu mnavyoweza kusimamia kwa umakini mambo yenye maslahi mapana kwa nchi yetu," alisema.

Dk. Nchemba aliridhia noti hizo ziingizwe kwenye mzunguko na kuanza kutumika kama ilivyopangwa Februari Mosi, mwaka huu.

# Waziri wa Afya aipa maagizo 11 Bodi NHIF

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Jenista Mhagama ameagiza Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuhakikisha Sheria mpya ya Bima ya Afya kwa Wote inatekelezeka na kukidhi matakwa na matarajio ya wananchi.

Jenista alitoa agizo hilo na mengine 11 jijini hapa juzi wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo.

Mengine ni bodi hiyo kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza wigo wa wananchi kufikiwa na mfuko huo ndani ya miezi sita.

Alisema moja ya jukumu analohitaji kuanza kusimamiwa haraka ni ufanisi wa sheria hiyo na kuwajibika ili usonge mbele.

"Wajumbe wa bodi mnayo kazi kubwa sana mbele yenu kuhakikisha mnashirikiana kwa karibu na Menejimenti, Katibu Mkuu wa Afya, Kamati ya Bunge kuhakikisha sheria mpya ya bima ya afya kwa wote inatekelezeka vyema na kukidhi matakwa na matarajio ya Watanzania," alisema.

Jenister, alisema bodi huiyo inatakiwa kutengeneza mifumo thabiti ya bima za afya kwa wote na kusisitiza watumishi wa mfuko wabebe usalama wa wananchi wote ili wapate huduma zote za msingi.

Alisema anatamani Tanzania ifikie hatua ya kutambulika na kuigwa na mataifa mengine duniani kwa uendeshaji mifumo ya bima kupitia mfuko huo.

"Bodi hakikisheni mnalinda mafanikio haya yaliyopatikana hivi sasa kwa wivu mkubwa na ziada ya mapato itumike vizuri," alisema na kuongeza kuwa: "Tumeshaondoka na tumefika mahali salama tukifanya hivyo mfuko utakuwa na akiba ya miaka 10 hadi 15, ni maamuzi ya uzalendo yanayoendana na taifa letu."

Kadhalika, aliagiza bodi hiyo itoe elimu kuhusu vifurushi vipya vilivyotangazwa hivi karibuni ili kukidhi malengo yaliyokusudiwa.

Alisema hadi Januari mwaka huu, serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imetoa Sh. trilioni 8.9 kwenye sekta ya afya.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, Elibariki Kingu, alishauri kuelekea utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Waziri Jenister akutane na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde ili kuwaunganisha wachimbaji wadogo na wakulima kupitia vyama vya ushirika kwenye mfuko huo na kuongeza wanachama.



Awali Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dk. Irene Isaka, alisema bodi iliyopita imeshiriki katika maandalizi ya Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote na kusimamia usajili wa wanachama kutoka milioni 1.2 mwaka 2020 hadi milioni 1.24 mwaka jana.

Irene, alisema bodi hiyo pia imeshiriki kuanzisha utaratibu wa kuhakiki wanachama na wastaafu, kuidhinisha kitita cha mafao, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuhamasisha wananchi umuhimu wa bima ya afya kwa wote.

Akizungumzia changamoto zilizoikabili bodi iliyopita, alizitaja kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za magonjwa yasiyo ya kuambukiza na kukosekana kwa utamaduni wa kuwa na bima kwa wananchi kabla ya kupata huduma.

Nyingine ni uhiari wa wananchi kujiunga na bima ya afya na kuchelewa kulipwa kwa fedha ambazo mfuko iliikopesha serikali na kuongezaka kwa gharama za kuwahudumia wastaafu.

Hata hivyo, alisema utendaji wa bodi mpya umesaidia kupunguza nakisi na kuongeza ziada ya mapato ya mfuko kutoka Sh. bilioni 47 hadi Sh. bilioni 111, usajili wa vituo na kupunguza muda wa uchakataji wa madai.

Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, alisema mfuko huo unachangia zaidi ya asilimia 80 ya huduma za bima nchini na sekta binafsi chini ya asilimia 20.

Saqware, alisema sekta ya bima imeendelea kukua na kuimarika nchini kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo sera nzuri zinazopitishwa na serikali.


ENTRY FREE VISIT
INTL TRADE EXHIBITION ON FOOD & PROCESSING
PLASTICS & PACKAGING - PAPER & TISSUE

EXHIBITORS FROM AROUND 17 COUNTRIES

FOODPACK 2025

Products on Display:
Biscuits & Confectionery | Cooking Oil | Cartons for Packaging | Dates Dairy & Milk Products | Premixes for Cakes | Premixes for Bakery Paper Disposable Products | Foam Disposable Food Containers Tissue & Napkins | Disposable Tableware | Plastic Food Containers Plastic Juice Containers | Packaging | Rice | Tomato Ketchup | Salt Silos | Vegetables & Fruits Processing Machinery | Water | Weighing Scale

INTERPLAST PACK
Products on Display:
- Air Compressors
- Boilers
- Glue
- Pneumatic
- Hose Reels
- Packaging
- Seasonal Giveaway's
- Reusable packaging
- Polypropylene (PP) Welding Machinery
- POS Materials
- Publishing
- Food Packaging
- Variable Data Printing
- Digital Printing Solution
- UV Printing Digital Solution
- Extruded Polypropylene
- Sheets
- Plastics Printing Plastics Houseware

PAPER & TISSUE
Products on Display:
- Tissue Converting Machines
- Mat Machines
- Paper Products
- Printing
- Packaging
- POS Materials
- Publishing
- Paper Disposable Products
- Foam Disposable Food Containers
- Food Packaging
- Variable Data Printing
- Digital Printing Solution
- UV Printing Digital Solution

Date & Venue
23-25 January 2025
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania

Timing
10:00 AM TO 6:00 PM

For more info, Please Call
0758 571652 / 0656 482557

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi wa CHADEMA umekwisha, kazi iliyobaki sasa ni kukijenga chama

**CHAMA** cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimemaliza uchaguzi wa viongozi wake wakuu katika mkutano mkuu uliofanyika kuanzia Januari 20 na kutamatika mapema jana.

Katika uchaguzi huo, mwanasiasa na mwanasheria machachari, Tundu Lissu, ameibuka mshindi katika nafasi ya mwenyekiti baada ya kumbwaga aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo kwa zaidi ya miongo mwili, Freeman Mbowe. Lissu alipata kura 513 sasa na asilimia 51.5 wakati Mbowe alipata kura 483 ambazo ni asilimia 48.3.

Naye aliyekuwa Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, amekuwa makamu mwenyekiti wa chama hicho kikuu cha upinzani akichukua nafasi ya Lissu aliyekuwa akiishikilia nafasi hiyo kabla ya uchaguzi.

Kwa kuangalia takwimu za matokeo hayo ya mwenyekiti, inaonesha dhahiri kwamba ushindani ulikuwa mkubwa kama ilivyoonekana wakati wa mnyukano wa hoja na kuwapo kwa makundi ya wafuasi wa pande mbili kabla ya kwenda kwenye sanduku la kura. Kwa maneno mengine, haikuwa rahisi kutabiri mshindi baina ya vigogo hao wa siasa ndani ya CHADEMA.

Baada ya matokeo kutangazwa na mshindi kujulikana, Mbowe aliandika katika mtandao wake wa X kuwa anakubali kushindwa na kumpongeza mpinzani wake kwa ushindi alioupata. Huo ndio uungwana wa kisiasa kwa mtu kukubali kushindwa badala ya kuanza kuibua nongwa ambazo zinaweza kukigawa chama na hata kuonesha kuwa mtu si mwanademokrasia kama anavyoinadi majukwaani.

Hatua hiyo ya ukomavu wa demokrasia ndani ya CHADEMA imepongezwa na watu wengi wakiwamo wanasheria na wanaharakati wa haki za binadamu kwamba umekuwa wa huru na wa wazi.

Mmoja wa wanaharakati waliopongeza hatua hiyo ni Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo-Bisima, aliyesema hatua iliyofikia CHADEMA katika uchaguzi huo ni ukomavu wa siasa kwa kuwa umekuwa wa amani. Zaidi ya hayo, amesema mshindi amepatikana na aliyeshindwa amekubali kushindwa na hiyo ndiyo maana halisi ya demokrasia.

Mwenyekiti huyo mteule kwa upande wake, baada ya kutangazwa mshindi alisema chama kimeweka kiwango cha dhahabu cha demokrasia ya ndani na kuvitaka vyama vingine vya siasa nchini kuiga mfano wao. Pia alibainisha kuwa uchaguzi ulikuwa wa wazi, huru na haki bila mizengwe japo alikiri kuwa kulikuwa na misuguano na kasoro za hapa na pale.


Katika kuonyesha kwamba wataendelea kuwa wamoja, Lissu alisema Mbowe ndiye aliyefanikisha uchaguzi huo kuwa katika hali hiyo na anastahili pongezi huku akiweka bayana kwamba historia ya chama itakapoandikwa, watu watatambua huu mchango wake mkubwa aliotoa. Pia alisema Mbowe hajastaafu bali ataendelea kuwa mjumbe wa kudumu wa kamati kuu ya chama kama katiba ya CHADEMA inavyoainisha.

Jukumu kubwa linalopaswa kufanywa na makundi hayo, yaliyokuwa yakijulikana kama 'Team Mbowe' na 'Team Lissu' ni kuungana na kuwa wamoja hatimaye kuendelea kukifanya kuendelea kuwa chama kikuu cha upinzani. Pia wana CHADEMA wanapaswa kuudhirihishia umma kwamba maneno yaliyokuwa yakienezwa kwamba chama kitasambaratika, zilikuwa ndoto za mchana na kwamba kitaendelea kuwa imara zaidi kuliko awali.

Pia viongozi, wanachama na wafuasi wa CHADEMA wanapaswa kutambua kwamba uchaguzi ndani ya chama umetamatika hivyo kazi iliyobaki ni kujijenga chama na kujiandaa na uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Oktoba, mwaka huu na hatimaye kushinda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kampeni ya Samia, itanusuru vifo vyao mapema wanaume

Na Adam Fungamwango

**NI** kama utamaduni uliorithiwa tangu enzi na mababu kuwa wanaume hawatakiwi kulalamika au kuongea sana. Ikasemekana kuwa hiyo ni tabia ya asili ya wanawake.

Hata hivyo, miaka ilivyozidi kusonga mbele, ikabainika kwa sayansi ya kitaalamu na zisizo za kitaalamu, kuwa wanaume hufa mapema kuliko wanawake.

Ndiyo maana unaweza kwenda kwenye vijiji mbalimbali ukakuta kuna wazee wengi wanawake kuliko wanaume.

Tatizo ni kwamba, tangu 'enzi na enzi', wanaume wameaminishwa kuwa wao ni wababe, pia viongozi wa familia.

Hivyo, wanakuwa hawapaswi kulia, kulalamika na hata kwenda sehemu kulalamika chochote ili kupatiwa ufumbuzi, badala yake wanatakiwa kukaa nacho rohoni na yeye mwenyewe ndiye aamue nini atafanya.

Jambo hilo limekuwa likiwatesa wanaume wengi miaka nenda rudi, matokeo yake wamekuwa wakifanya maamuzi mengine ya ovyo, ukatili wa kijinsia na kijamii, kujinyonga, na hata kupata ugonjwa wa sonona ambao unawafanya wafe mapema kuliko wenzao. Kampeni mbalimbali duniani zikaanza kufanywa ili kuondoa hali hiyo ambayo mwanzoni ilionekana kuwa ngumu kutokana na mazoea.

Kila miaka inavyozidi kwenda baadhi ya wanaume wanabadilika na kukubali kuwa kuna wakati inabidi watoe walichonacho moyoni ili wasaidiwe kupatiwa ufumbuzi wowote, ikiwamo wa kisaikolojia.

Juzi, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, aliwashangaza wengi alipotangaza kuwa wanaume wanaongoza kujitokeza kutoa malalamiko yao kwenye Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Akizungumza jijini Dodoma, msomi wa sheria Dk. Ndumbaro, akasema jumla ya wananchi 775,119, wamehudumiwa katika kampeni hiyo kwenye mikoa 11, huku wanaume wakiongoza kujitokeza kutoa kero na malalamiko yao.

> **Matatizo ni kero na binadamu anapoishi duniani, huwa hayaepukiki, lakini yanapaswa kuelezwa kwa kupelekwa kwa watu husika ili kupata ushauri, uwe wa kidaktari, kimawazo, kisaikolojia ili kumrudisha kwenye hali ya kawaida.**

Lingine akataja kwamba,wanaume waliotoa malalamiko yao kwa asilimia 51 na asilimia 49 ikibaki kwa wanawake.

"Hayo ni mafanikio makubwa kutokana na kuwasaidia wanaume kufikisha kero zao. Naomba na wengine kujitokeza kutoa kero zao kwa sababu ni siri ya mhusika na mtoa huduma ya kampeni tu," akasema.

Kwa hali ya kawaida, isingeweza kutokea kitu kama hicho miaka kadhaa nyuma. Wanaume wamekuwa hawawezi kufanya hivyo na si kama hawana matatizo, bali aibu ambayo imejengwa na jamii huko nyuma juu ya wanaume.

Lakini, kwa wakati mwingine inawezekana kuwa wanaume wana matatizo mengi zaidi kuliko hata wanawake, ila yamekuwa hayajulikani kwa sababu ya kujificha kwenye kichaka cha uanaume.

Wanaume wanabeba mambo mengi ya kifamilia, kijamii, kiuchumi, kimahusiano na mengine yanayofanana na hayo, kimoja kikiyumba tu, kwake ni matatizo makubwa.

Matatizo ni kero na binadamu anapoishi duniani, huwa hayaepukiki, lakini yanapaswa kuelezwa kwa kupelekwa kwa watu husika ili kupata ushauri, uwe wa kidaktari, kimawazo, kisaikolojia ili kumrudisha kwenye hali ya kawaida.

Tunapongeza kampeni hiyo ya Mama Samia na inatakiwa kuendelea kusaidia wananchi, wakiwamo wanaume wanaonekana kuiamini na kumiminika kutoa malalamiko yao.

Kama alivyosema Dk. Ndumbaro kuwa wasiogope, kwani hakuna kitu kinakachotoka nje ni siri, kwamba kampeni hiyo itaendelea na kuvuta wanaume wengi, ikiwapatia msaada unaohitajika na kupunguza vifo vya mapema kwao.

Mara nyingi, vifo hivyo vinatokana na kuweka vitu moyoni bila ya kuwashirikisha wengine au wataalamu. Badala yake, vinaendelea kumtesa moyoni hadi kuathiri afya zao, ikiwamo kusababisha vifo.

HABARI KITAIFA

# Karatu yafikiwa na elimu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu,** KARATU

WANANCHI wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha wameshauriwa kutumia taasisi za fedha zilizosajiliwa ambazo zinazingatia sheria, kanuni na taratibu katika huduma za fedha ili kujiepesha na watoa huduma za fedha wasiosajiliwa.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, alitoa rai hiyo juzi alipokutana na timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha waliofika hapa kutoa elimu ya fedha kwa wananchi ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa wizara kuwawezesha wananchi kuwa na uelewa wa masuala ya fedha.

Kolimba alisema kumekuwa na baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo kwa wananchi ambazo hazifuati sheria, hivyo kusababisha malalamiko ya mara kwa mara na wananchi kupoteza mali zao ambazo wameweka dhamana.

"Tulishazungumza na watoa huduma za fedha na taasisi za fedha hapa wilayani na tukasisitiza kuwa mikopo wanayotoa isiwaumize wananchi na tukigundua wanakwenda kinyume cha sheria tutawachukulia hatua za kisheria. Tunasisitiza wananchi kutumia watoa huduma rasmi za fedha ili kuepuka mikopo isiyofuata sheria," alisisitiza.

Kuhusu elimu itakayotolewa na wataalamu wa Wizara ya Fedha, alisema itawasaidia kupata uelewa wa haki na wajibu wa mtoa huduma katika utoaji wa mikopo ili kuwasaidia kuondokana na mikopo umiza.

Kolimba alisema ana imani elimu itakayotolewa kwa wananchi itawaongezea uelewa zaidi wa kutambua haki zao ikiwamo kufahamu taratibu za mikopo ikiwamo kiasi cha riba watakachotozwa na taasisi ya fedha katika mikopo wanayochukua kabla ya kuchukua mkopo.

'Natoa pongezi kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo haya ya kutoa elimu kwa wananchi na pia nimpongeze Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maelekezo haya kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi ili kuondokana na changamoto za kiuchumi," aliongeza.

Kolimba pia alisisitiza wananchi wilayani Karatu kuhakikisha wanapochukua mikopo kwa wenye wenza, wawashirikishe ili inapotokea changamoto katika urejeshaji, washirikiane kurejesha lakini pia kuepuka migogoro ya familia endapo mwenza asiposhirikishwa na mkopaji akishindwa kurejesha mkopo kwa wakati.

Kuhusu programu ya elimu ya fedha kwa wananchi wa Wilaya ya Karatu, Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, alisema wizara inatekeleza programu hiyo ili kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha wananchi kutumia huduma rasmi za fedha.



Mfanyausafi akisafisha kuondoa taka katika mfereji wa maji ya mvua, kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mwaka 2024 wavunja rekodi joto kali duniani

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema mwaka 2024 umevunja rekodi kwa ongezeko la joto duniani likiongezeka kwa nyuzi joto 1.55.

Akizungumza kwenye warsha ya wanahabari juu ya Utabiri wa Mvua za Msimu wa Masika, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema ongezeko hilo ni la dunia huku kwa Tanzania joto likiongezeka kwa nyuzi joto 0.7 likiwa ni ongezeko la juu zaidi kurekodiwa.

"Hii yote inatokana ma mabadiliko ya hali ya hewa ambayo dunia inakutana nayo. Kwa rekodi kuanzia mwaka 2023, inaonesha joto litaendelea kuongezeka zaidi duniani," alisema Dk. Chang'a.

Kutokana na hali hiyo, alisema juhudi zaidi zinatakiwa katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani kote.

Katika hatua nyingine, Dk. Chang'a aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwekeza kwenye sekta ya hali ya hewa katika miundombinu na rasilimali watu.

"Katika kupindi cha mwaka jana, serikali imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa rada mbili katika mikoa ya Kigoma na Mbeya. Hii inafanya kwa Afrika Mashariki kuwa nchi kinara kwenye miundombinu ya hali ya hewa," alisema Dk. Chang'a.

Kwa upande wa ujuzi, alisema mamlaka hiyo ina wafanyakazi 560 na kati ya hao, 80 wako mafunzoni ndani na nje ya nchi sawa na asilimia 15 ya wafanyakazi wote.

"Kwa uwekezaji huu unatupa fursa wa kuendelea kuwa kitovu cha ubora katika masuala ya hali ya hewa Afrika. Sababu za kuwa hivyo tunazo na uwezo pia tunao kutokana na uwekezaji unaofanywa na serikali, hili nimelisema mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akizindua mradi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani wa 'Systematic Observation Fanancing Facility' kule Dodoma, jana (juzi)", alisema.

Wakati huo huo, TMA imetoa wataalamu wawili wa hali ya hewa kwenda Burundi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu wa nchi hiyo.

Alisema wenzao wa Burundi wameomba kupatiwa wataalamu hao ili kuwajengea uwezo wafanyakazi wao mamlaka ya hali ya hewa ya nchi hiyo.

"Tunatarajia wataalamu wetu wawili kesho (leo) wataenda Burundi baada ya maombi ya wenzetu. Hii inaonyesha ni namna gani tumekuwa na wataalamu wengi kutokana na uwekezaji wa serikali katika kuwajengea uwezo wataalamu wa TMA," alisema Chang'a.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# Askari kizimbani madai mauaji ya kijana

**Na Francis Godwin, IRINGA**

ASKARI polisi mmoja na askari wa jeshi la akiba (mgambo) wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa na kusomewa shtaka la mauaji ya kijana Nashon Kiyeyeu.

Washtakiwa hao ni askari polisi wa Kituo cha Ipogolo, Rojas Mmali na mgambo Thomas Mkembela.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani juzi saa 7:00 mchana huku ulinzi ukiwa umeimarishwa katika viwanja vya mahakama.

Akisoma maelezo ya kosa, Wakili wa Serikali, Damas Sixtus alisema kuwa washtakiwa hao walimuua Kiyeyeu Desemba 14, mwaka jana, katika eneo la Ipogolo.

Hata hivyo, wakili huyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu Mkazi Mfawidhi, Adelina Ngwaya, alisema washtakiwa hao hawatakiwi kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji.

Washtakiwa hao hawakupewa dhamana na kurudishwa rumande hadi Februari 4, mwaka huu, kesi itakapotajwa.



Askari Polisi namba F4987 Sajini Rojas Joshua Mmali (aliyejificha sura) na askari wa jeshi la akiba (mgambo), Thomas Mkembela (kulia), wakiwa chini ya ulinzi, walipofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa juzi, kusomewa shtaka la mauaji ya kijana Nashon Kiyeyeu. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Biteko ataka mitaala iboreshwe

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO vikuu na vya kati nchini vimetakiwa kuboresha mitaala yake, ili kutoa wahitimu wanaokidhi mahitaji ya soko la ajira la sasa na kutumia teknolojia ya kisasa katika kujibu changamoto zinazoikabili jamii.

Wito huo ulitolewa juzi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya kuanzishwa kwa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), yaliyofanyika kampasi kuu ya Dar es Salaam.

Alisema serikali inavitaka vyuo hivyo kuweka mkazi wa mafunzo ya ujasiriamali, ili wahitimu wake waweze kuwa na ujuzi wa biashara na kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa kupitia biashara bunifu na ajira binafsi.

Dk. Biteko alisema vyuo kama CBE vinawajibu wa kudumisha uhusiano wake na sekta binafsi, ili waweze kufahamu soko linahitaji wahitimu wa aina gani badala ya kujifungia na kufanya mambo binafsi.

Dk. Biteko alisema serikali inahimiza vyuo vya elimu ya biashara kufanya tafiti za kina zinazosaidia kutatua changamoto za kiuchumi na kubuni suluhisho endelevu kabla ya matatizo hayajatokea kwenye jamii.

"Tumeelekeza vyuo kama CBE kuhakikisha fursa za elimu zinawafikia maakundi yote ya jamii kama wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kujumuisha watu wote kwenye uchumi wa taifa letu," alisema.

Alimpongeza Mkuu wa chuo hicho, Profesa Edda Lwoga na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo kwa kuendelea kusimamia chuo hicho na kuwatoa wahitimu bora wanaokidhi mahitaji ya soko.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema kwenye awamu ijayo ya mradi wa upanuzi wa vyuo vikuu (HEET), serikali itahakikisha CBE kinaingizwa kwenye orodha ya vyuo vinavyostahili kupewa fedha.



Alisema kwa miaka 60 tangu kuanzishwa kwake chuo hicho kimekuwa chachu ya maendeleo ya biashara nchini kwa kutoa maelfu ya wahitimu ambao wamekuwa wakifanyakazi katika sekta ya umma na binafsi.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, alisema chuo hicho kimekuwa kikiendeleza uhusiano na mataifa mbalimbali duniani kama Ujerumani, Finland na China.

Alisema uhusiano huo umekuwa msaada mkubwa kwa wahadhiri wa chuo hicho kwenda kujengewa uwezo katika maeneo mbalimbali na wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kwa kwenda kujifunza kwenye vyuo vya nchi hizo.

"Kwenye eneo la vipimo, viwango na kidijitali kazi kubwa inaendelea kufanywa na chuo hiki na CBE imekuwa ni ufunguo wa biashara na takwimu ulimwenguni zinaonyesha kuwa watu wengi na hapa nchini wamejikita kwenye biashara na wengi wamepitia chuo hiki," alisema.

Alisema chuo hicho kimekuwa kikiwapa elimu ya ujasiriamali wafanyabiashara wadogo wadogo wa mkoa wa Dar es Salaam ambapo mpaka sasa zaidi ya wajasiriamali 3,000 wamenufaika.

Mkuu wa chuo hicho, Profesa Edda Lwoga alisema chuo kimepiga hatua katika udahili ambapo jumla ya wanafunzi 22,335 wamedahiliwa katika kampasi zake za Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Mbeya.

Alisema chuo kimefanikiwa kupanua programu zake kutoka katika ngazi ya astashahada hadi ngazi ya Shahada za Uzamili na kwamba hivi sasa chuo kinatoa jumla ya programu 63 zinazojumuisha ngazi ya cheti, diploma, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Umahili.

Alisema ili kuhakikisha wanawafikia watu wengi wenye sifa stahili kwa ajili ya Shahada za Umahiri, CBE imeboresha mitaala yake ambapo wameanza kutoa mafunzo ya shahada za uzamili kwa njia ya mtandao (online masters).

## Mlalamikaji kesi bastola achelewa kufika kortini

**Na Grace Gurisha**

KESI ya inayomkabili Derick Junior (36) ya kutembea na silaha hadharani kinyume cha sheria na kumjeruhi Julian Bujulu, imekwama kuanza kusikilizwa.

Kesi imeshindwa kuanza kusikilizwa baada ya mlalamikaji kuchelewa kufika mahakamani kwa muda uliopangwa.

Bujulu alitakiwa kufika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Is-haq Kuppa saa 5:00 asubuhi, ili aanze kutoa ushahidi wake, ambapo yeye ndiye shahidi wa kwanza kwa upande wa Jamhuri katika kesi hiyo.

Hakimu Kuppa alipanga kusikiliza kesi hiyo kuanzia saa tano kamili asubuhi hadi saa sita na nusu mchana, lakini alilazimika kuahirisha kesi hiyo kwa sababu ya mlalamikaji wa kesi hiyo (Bujulu) kutokufika ndani ya muda uliopangwa.

Hakimu alishindwa kuisikiliza kesi hiyo kwa sababu tayari alishapanga muda kwamba akishamaliza kusikiliza ndipo aende kwenye maandalizi ya siku ya sheria kwa sababu na yeye ni sehemu ya kutoa elimu shuleni kwenye siku hiyo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 5 na 6, 2025, itasikilizwa mfululizo saa tano asubuhi, mlalamikaji anatakiwa kufika mahakamani mapema ili kufuata muda ulipangwa na mahakama.

Kwa upande wa Jamhuri katika kesi hiyo unawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Sada Mohamed na utetezi Jeremiah Mtobesya.

Junior ameachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya kuwa na mdhamini mmoja wa kuaminika aliyesaini bondi ya Sh. 8,000,000.

Awali, akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Dickson Swai alidai kuwa mshtakiwa huyo anatuhumiwa kwa mashtaka mawili likiwamo kusababisha jeraha kubwa kwa mtu.

## KANDA KASKAZINI



# Taharuki mazao ya wakulima kukauka

**Na Allan Isack,** ARUMERU

ZAIDI ya ekari 1,000 za mazao katika Kijiji cha Makiba Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha zimekauka kwa ukame kutokana na kukosa maji kwa ajili ya umwagiliaji ya mfereji wa Makiba.

Kwa miaka kadhaa, mfereji huo umekuwa tegemeo kwa wakulima zaidi ya 5,000 wa kijiji hicho na vya jirani wa mazao hayo ya mahindi, maharage, migomba, mihogo na mboga.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakulima, akiwamo Athanas Sumari, alisema hali ya maisha yao kwa sasa ni mbaya baada ya mazao yao kukauka.

**Suala hili nimelifikisha kwenye Ofisi ya Ofisa Tarafa ya Mbuguni kwa ajili ya kufuatilia na kuchukulia hatua zaidi kwa waliosababisha maji kufungwa.**

Sumari, alisema baadhi ya watu wenye nguvu kuliko wao, wamefunga maji hayo ya mfereji na kuyatumia kwenye mashamba yao makubwa na kusababisha mazao yao kukauka.

"Hali ni ngumu kweli kweli kwa upande wetu wakulima kwa kuwa mazao yetu yamekauka na hatua zisipochukuliwa athari itakuwa kubwa na tutaathirika kabisa," alilalamika.

Mkulima mwingine, Joseph Justo, alisema wamepanga kuandamana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kufikisha kilio chao cha kukatiwa maji.

Justo, alisema baadhi ya wakulima wakubwa kwenye mashamba yaliyoko Doli, wamefunga mfereji huo unaotiririsha maji kwenda kwenye mashamba yao na kuathiri mazao yao kwa kukauka.

Pius Mmassy, alisema baadhi yao wamechukua mikopo benki na taasisi za fedha na kwamba anaona dalili ya kushindwa kurejesha mkopo kwa kuwa mazao yake yamekauka kwa ukame.

"Tunaomba serikali iingilie kati suala hili kwa kuwa wakulima tutakuwa masikini kutokana na mikopo tuliyoichukua tutashindwa kuilipa nani kutaifishwa mali zetu," alisema.

Katibu wa mfereji huo katika eneo la Makiba, Elieza Kisaka, alisema kuna mtumishi wa idara ya umwagilia wa wilaya hiyo (hakumtaja jina), alitoa maelekezo ya maji kufungwa katika mfereji huo.

Kisaka, alisema mtumishi huyo, amesababisha maji yanayotiririka kutoka mfereji wa Doli hadi Kijiji cha Makiba kukatwa na kuzua taharuki hiyo kwa wakulima hao kwa mazao ya kukauka.

Alipotafutwa kuzungumzia suala hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Makiba, Godlisten Lema, aliwapongeza wakulima hao kudai haki zao kistaharabu kwa kufuata hatua bila kufanyiba uharibifu wowote.

"Suala hili nimelifikisha kwenye Ofisi ya Ofisa Tarafa ya Mbuguni kwa ajili ya kufuatilia na kuchukulia hatua zaidi kwa waliosababisha maji kufungwa," alisema Lema.

Diwani wa Kata ya Makiba, Samson Laizer, alisema ili kuhakikisha changamoto hiyo inapatiwa ufumbuzi inatakiwa mapendekezo manne yaliyotolewa yafanyiwe kazi.

## 'TAWJA yahitaji mahakimu, majaji wanawake wa kutosha'

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma amesema Chama cha Mahakimu na Majaji, Mahakama ya Tanzania (TAWJA), kinahitaji kuwa na idadi ya kutosha ya mahakimu na majaji wanawake.

Akizungumza juzi jijini hapa wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Miaka 25 ya TAWJA, Prof. Juma, alisema historia ya mahakama nchini kwa kipindi cha mwaka 1921-1961, haikutoa nafasi za ajira kwa majaji na mahakimu wanawake.

Alisema hatua kubwa imefanywa na serikali kuongeza idadi ya wanawake katika utumishi wa mahakama, lakini bado ina safari ndefu kufikia asilimia 50/50 ya idadi ya wanawake na wanaume katika nafasi hizo.

Prof. Juma, alisema kwa mujibu wa takwimu ya Msajili Mkuu wa Mahakama, Januari 15 mwaka huu, ajira za kila mwaka kati ya mwaka 2000 (TAWJA ilipoanzishwa), hadi Disemba mwaka jana, serikali iliiwezesha Tume ya Utumishi wa Mahakama kuajiri mahakimu 1,441.

Kwa kipindi cha miaka takriban 25, tume hiyo iliajiri mahakimu wanawake 688 sawa na asilimia 48.

Idadi ya mahakimu wanaume walioajiriwa katika kipindi hicho, walikuwa 753 sawa na asilimia 52 na kwa mwelekeo wa ajira ya mahakimu wanawake ni kwenye usawa asilimia 50, au zaidi kwa kuwa kwa miaka ambayo ajira ya mahakimu hao ilizidi ile ya mahakimu wanaume.

Katika Mahakama ya Rufani, idadi ya majaji wanawake imefikia asilimia 33 na Mahakama Kuu 38, huku wasajili wa mahakama asilimia 33.

Naibu wasajili ni asilimia 48.7, ambapo wanawake ni asilimia 50 kwa mahakimu na mahakimu wakazi, huku 41 ikiwa ni nahakimu wa mahakama za mwanzo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert (katikati), akizungumza na viongozi wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) wa mkoa wa Tabora na Kanda ya Magharibi, walipofika katika ofisi za shirika hilo, mjini Tabora juzi, kubadilisha mawazo ya jinsi ya kuwainua kiuchumi vijana, wanawake na makundi maalum. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadamka kufuata huduma za ardhi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MIGOGORO ya ardhi mkoani Kilimanjaro imeendelea kubadili taswira ya wakazi wake, kutokana na kuongezeka kwa thamani ya ardhi kwa kumiminika alfajiri kufuata huduma za kisheria Baraza la Ardhi la Mkoa huo.

Jana, Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu (pichani), kabla ya kuzindua kliniki ya sheria bila malipo na kamati ya ushauri wa kisheria ya mkoa, alisema changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi, inamshangaza.

"Mkoa huu changamoto kubwa ni ardhi. Ukienda hapo ofisi ya ardhi wanasema baraza; yaani nikiingia mpaka nashangaa, watu saa 11 wamejaa hapo. Yaani mtu wanagombania hata robo hatua, lakini hamuachii mwenzake. Sasa hiyo ndio Kilimanjaro. Ardhi hapa ni shughuli pevu," alisema Babu.

Alisema Kamati ya Ushauri ya Kisheria zimeanzishwa kwa mujibu wa mwongozo kuwasaidia wananchi, watumishi wa umma na viongozi wa umma kutatua changamoto zinazojitokeza katika mkoa huo na wilaya zake.



"Serikali imekuja na kliniki ya bure ya kisheria, hutakiwi kutoa hata shilingi moja. Niwaombe wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, wajitokeze kwa wingi katika kliniki iliyoanza Januari 21 mpaka 27 mwaka huu," alisema.

Alisema huduma hiyo itasaidia kupunguza malalamiko ya kisheria kwa wananchi.

Awali, Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Tamari Mndeme, alisema wamejenga kutoa huduma za kisheria bure kwa wananchi kupitia kliniki hiyo.

"Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,iko tayari kuwahudumia wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, tuna wataalamu wa kutosha, tunaamini kupitia kliniki hii changamoto mbalimbali za wananchi zitatatuliwa," alisema Tamari.

Kliniki ya sheria bila malipo kwa wakazi wa mkoa huo ni mwendelezo wa Ofisi ya CAG kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi.

Huduma hizo zinatolewa katika eneo la stendi ya vumbi jirani na Kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani mjini Moshi.



# Radienya; shule yenye miundombinu mibovu

**Na Vitus Audax**

MAISHA ya wanafunzi zaidi ya 600 wa Shule ya Msingi Radienya iliyopo Kata ya Kirogo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara yako hatarini kutokana na ubovu wa madarasa.

Licha ya ubovu wa madarasa hayo saba, shule hiyo ina walimu watano, mmoja akiwa nje ya kituo cha kazi kwa masomo, mazingira na miundombinu ya barabara mibovu na kufika kwa shida.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Rwehumbiza Tryphone, aliwasilisha changamoto hizo juzi wakati wa ziara ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Gerald Kusaya.

Tryphone, alisema kati ya madarasa hayo saba, moja ambalo hali yake ni nzuri limejengwa kwa nguvu ya wananchi na kusaidiwa na serikali.

**Tatizo ukiingia kwenye mfumo, shule hii inaonyesha mambo yake yapo safi, ina vyoo, madarasa ya kutosha na nyumba za walimu.**

Alisema shule hiyo ina matundu manne ya vyoo ambayo hayakidhi matumizi ya wanafunzi hao kutokana na wingi na kwamba yapo katika hali mbaya, hivyo kuzidi kuhatarisha afya za wanafunzi hao.

Tryphone, aliendelea kusema kuwa, shule hiyo ina nyumba sita za walimu, kati ya hizo mbili ni mbovu, hivyo hazifahi kuishi ni nne ni chakavu.

Akizungumza baada ya kukagua na kubaini ubovu wa miundombinu hiyo ya shule hiyo, Kusaya, licha ya kuwapongeza walimu kwa uvumilivu wa mazingira hayo magumu, aliagiza idara husika kuchukua hatua haraka kukabiliana na hali hiyo.

"Shule hii tutaifanyia maboresho makubwa hivi karibuni na hususan miundombinu ili mazingira yawe rafiki kwa walimu na wanafunzi na kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha," alisema.

Kusaya, alianza kwa kumwagiza Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa mkoa huo kufuatilia kwa maboresho yanayohitajika katika shule hiyo kwa kuwashirikisha wadau wa elimu na kutumia vizuri fursa zinazotolewa na serikali.

Vilevile, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Abdul Mtaka kutembelea shule hiyo na kuwasilisha mahitaji halisi ya shule hiyo ofisini kwake na hatua halmashauri hiyo itachukua haraka ili iendelee kutumika wakati fedha za ujenzi wa shule mpya zinatafutwa.

Alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Mkoa huo, kutembelea shuleni hapo, kujenga barabara na daraja kuweza kupitisha magari na wanafunzi wakati wa kuingia na kutoka kabla na baada ya masomo.

Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Elimu, Makwasa Bulenga, alisema Idara ya Elimu ya Halmashauri hiyo, imehamishia walimu wawili wengine katika shule hiyo kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa watumishi hao unaoikabili.

Bulenga, alisema barua za uhamisho za walimu hao zipo tayari na wanatarajiwa kuwasili shuleni hapo hivi karibuni.

"Tatizo ukiingia kwenye mfumo, shule hii inaonyesha mambo yake yapo safi, ina vyoo, madarasa ya kutosha na nyumba za walimu," alisema.

"Lakini ukija hapa kuona hali halisi kuna darasa moja tu zima, majengo mengine yote ni mabovu hili ni tatizo linalosababishwa na walimu kutokufanya mabadiliko kwenye mifumo," aliongeza kusema Bulenga.

## Wafugaji samaki waiangukia TIC

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

WAFUGAJI wa samaki kwa njia ya vizimba wa Ziwa Victoria wamekiomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kutatua kero zao ili waweze kufanya uwekezaji katika mazingira rafiki na wezeshi.

Ombi hilo lilitolewa juzi wilayani hapa Mkoa wa Mwanza na Ofisa Rasilimali Watu na Utawala wa Kampuni ya Uwekezaji Samaki kwa njia ya vizimba ya Big Best, Simon Nzumbi wakati akiwasilisha kero zinazowakabili kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TIC, Dk. Binilith Mahenge.

Nzumbi, alizitaja baadhi ya kero hizo kuwa ni kukatika kwa umeme mara kwa mara, kuvamiwa kwa maeneo tengefu na wavuvi kisha kuvua samaki bila kibali na ufinyu wa maeneo ya kuchimba mabwawa ya kufugia samaki.

Nyingine ni chakula kwa ajili ya uzalishaji samaki kutoka nje ya nchi kuuzwa kwa gharama kubwa na kuchelewa kwa makontena ya vifaa vya mradi kutolewa bandarini licha ya mawakala kulipwa fedha zao kwa wakati.

"Pia tuna upungufu wa eneo la mita za mraba 20,000 umekuwa kikwazo katika matarajio yetu ya kuzalisha tani 900 hadi 1,200 za sato kwa mwezi ifikapo mwaka 2026," alisema Nzumbi.

Alisema mpaka sasa, wamepandikiza vijiti 1,000,000 kwenye vizimba vikubwa na kuanza kuvunwa Julai mwaka huu baada ya samaki kukomaa.

Alisema wanatarajia kuwa na jumla ya vizimba na vizimba vitalu 200 kutoka 112 vya sasa ifikapo mwaka 2026.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa madarasa ya sekondari mpya ya Kijiji cha Butata, Kata ya Bukima, Musoma Vijijini, mkoani Mara jana. Sekondari hiyo, inatarajiwa kufunguliwa mwezi ujao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CCM Sirari wamtumbua m'kiti wao kwa ukabila

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Sirari wilayani hapa Mkoa wa Mara, kimemsimamisha uongozi mwenyekiti wake wa Tawi la Sokoni, Rhobi Samwel kwa tuhuma za kuendekeza siasa za ukabila kwenye kura za maoni.

Inadaiwa kuwa Rhobi alifanya ubaguzi wakati wa kuwapata wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa jana kwa aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti Kijiji cha Sokoni, Erasto Benjamin kwa kumuita 'Mjaluo'.

Uamuzi huo wa kumsimamisha uongozi wa tawi hilo, ulifikiwa katika kikao cha kamati ya siasa ya kata hiyo kilichoketi mjini Sirari chini ya Mwenyekiti wa Kata wa CCM, Kelvin Masyaga baada ya wajumbe kwa kauli moja waliridhika nao.

Katibu wa CCM Kata ya Sirari, Mallson Haruna, alisema kiongozi huyo pia alituhumiwa na kikao hicho kuvujisha siri za chama kwa wapinzani na kutoshiriki kikamilifu kampeni za kuwanadi wagombea wa chama hicho katika kinyang'anyiro hicho mwaka jana.

"Imebainika mara kadhaa amekuwa akisambaza mambo ya chama nje hadi kwa wapinzani hasa maeneo la kucheza bao huku akirekodi matukio ya vikao kwa matumizi ya hila," alisema Haruna.

Alisema tayari mhusika amepewa barua ya maamuzi hayo na kusubiri hadi pale itakapoamuliwa vinginevyo na vikao vya juu.

Hata hivyo, alisema amepewa nafasi ya kukata rufani kupinga uamuzi huo wa kusimamishwa uongozi iwapo hakuridhika.

Alipotafutwa na Nipashe ili kujibu tuhuma hizo na uamuzi huo dhidi yake, Rhobi alipinga akidai hakupewa nafasi ya kujitetea na kuahidi kukata rufani ngazi ya wilaya ya chama hicho.

"Sitambui uamuzi huo kwa kuwa ulichukuliwa pasipo mimi kuhudhuria kikao wala sikupewa nafasi ya kujitetea dhidi ya tuhuma hizo za uongo ambazo zimetungwa kunichafulia jina, nitapinga uamuzi huo ngazi za juu wilayani," alisisitiza.

Alisema yeye bado ni mwenyekiti halali wa tawi hilo kwa kuwa alipata ridhaa kutoka kwa wanachama na ndio wana mamlaka ya kuamua si vinginevyo.

Akizungumza na Nipashe, Masyaga alisisitiza kuwa maamuzi yoyote dhidi ya mwanachama aliyekiuka maadili yanachukuliwa katika vikao halali.

"Chama chetu kinafanya kazi zake za kila siku za utekelezaji wa ilani yake kwa kuzingatia taratibu na maamuzi yoyote yanachukuliwa katika vikao halali sio nje ya hapo kama vile mitandaoni," alisema.

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI JANUARI 23, 2025




## Vitambue vipaumbele vitano siku zote vinavyolinda afya ya akili

Ukurasa 13



## MKAKATI KUUFUATA UMMA ULIKO... Anakokanyaga Samia kukabili shida afya akili, ziliko nyayo zao wananchi

Ukurasa 12

## FOLENI ZAHANATI WANAOGUA TUMBO...

# Uchache vyanzo maji, shida usimamizi unavyoacha rehani afya za wanavijiji

**Na Christina Haule, aliyekuwa KILOSA**

KILIO cha usimamizi usioridhisha wa Sera ya Maji ya Mwaka 2002, sasa una madai ya kuathiri upatikanaji wa majisafi kwa wakazi wa Kata ya Msowero, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro.

Ni hali inayotajwa kuchochea ongezeko la magonjwa ya tumbo, kuhara na kipindupindu, huku ikiathiri uchumi katika sekta za kilimo na maisha ya kila siku ya wakazi wa eneo hilo.

Kukirejewa taarifa za Zahanati ya Msowero, idadi ya wagonjwa waliopata magonjwa ya tumbo imeongezeka kutoka 1,211 mwaka 2022/23 hadi 1,502 mwaka uliofuata 2023/24.

Wagonjwa hao wengi wanatajwa kutoka katika vijiji na shule za sekondari, katika Kitongoji cha A-Mzanini na Mzambarauni, ambavyo vyote havina huduma za maji safi.

Ofisa Tabibu wa zahanati hiyo, Ramadhani Mnyanga, anasema huwa wanapokea wagonjwa 27 wanaougua, shida zinazoambatana na tumbo kila wiki.

Ingawa inatajwa kuwapo juhudi za kuelimisha jamii juu ya usafi zinaendelea, bado kunalalamikiwa kuwapo mitazamo hasi kuhusu matumizi ya maji ya kuchemsha au yaliyotiwa dawa, hata kusababisha changamoto kubwa.



Wanakijiji wa Kilosa, mkoani Morogoro wakichota maji katika vyanzo vyao. **PICHA: CHRISTINA HAULE.**

### MAISHA KILA SIKU

Wakazi wa Msowero, kwa kawaida hulazimika kutembea umbali wa kilomita tano hadi sita, kutafuta maji kutoka kwenye bomba lililoko kijijini Msowero.

Hapo inatolewa ushuhuda wa Theresia Muga, mkazi wa Kitongoji A-Mzanini, anasema wanalazimika kutumia baiskeli kufuata maji.

Hapo anafafanua kwamba, ni jambo linalochukua saa tano hadi nane kila siku.

Vilevile, adha hiyo anaitaja inawalazimu kuchota na kutumia maji ya Mto Msowero na pengine ya visima, ambayo sio safi wala salama na kusababisha migogoro ya kifamilia na kuhatarisha usalama wa wanawake na watoto.

Jenipher Jackson, ni mkazi wa kijiji hicho anayeeleza kuwa, maji wanayotumia yanatoka kwenye visima visivyo salama, kutokana na kubaki wazi.

Poa anataja maji hayo yakachanganyika na taka mbalimbali kama nywele na kinyesi cha mifugo, hali inayowaweka kwenye hatari kubwa ya magonjwa.

"Maji tunayochota, kisima kipo wazi, hakina mfuniko. Wakati mwingi tunapata maji yenye mavumbi yenye uchafu wa mifugo na matambara machafu, licha ya kwamba hayakidhi mahitaji ya wakazi wote tuliopo hapa na hivyo kutuweka kwenye wakati mgumu kiafya," analalamika Jenipher.

### WAKWAMA KISERA

Diwani wa Kata ya Msowero, Eliud Malekela, anasema utekelezaji wa sera ya kisiasa ya maji inayogota mwaka huu, kwao imefika nusu safari, yaani asilimia 50 pekee.

Safari waendako, anajitetea kwamba wanajipanga na mamlaka ya kiserikali inayosimamia huduma za maji - RUWASA kufanikisha safari yao, akitaja maeneo makongwe yasyofikiwa na mradi huo: Majamba, Mkogwe na Kitongoji cha Mzambarauni.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Msowero, Goodluck Magembe, anasema changamoto ya maji ilikuwa kubwa zaidi kati ya mwaka 2000 na 2019.

Anarejea kuwa, hali iliboreka kidogo kiasi, baada ya mradi binafsi uitwao Waridi ulipoanzisha vituo 26 vya kuhudumia maji.

Hata hivyo, anasema kiwango cha maji kilichoko, hakitoshelezi mahitaji ya wakazi, hivyo anaiomba serikali kuwasaidia mabomba ya visima vifupi 29.

Anafafanua kuwa, yakisambazwa kwenye maeneo yaliyokosa maji, yatasaidia kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa maji kulingana na mahitaji ya maji ya wakazi wa kijiji hicho.

Pia, anadokeza hatari inayowakabili iwapo jitihada zaidi hazitachukuliwa mapema kunusuru wakazi hao, kwamba wanaweza kuathirika kwa kupata magonjwa ya milipuko.

Anasema, maambukizi yakiwafikia itakuwa rahisi kwao kuambukizana, kutokana na mwingiliano walio nayo katika mahitaji na ununuzi wa vyakula, pia shughuli za kilimo cha mpunga na biashara ya mchele walio nayo.

Magembe anavitaja vijiji vinavyokabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji kuwa ni vitatu kati ya vinne vilivyopo kwenye Kata ya Msowero, vinajumuisha Mkogwe, Majambaa na Mambegwa, pia vitongoji kadhaa kutoka kwenye Kijiji cha Msowero.

### RUWASA NA CHANGAMOTO

Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kilosa, Mhandisi Silvia Ndimbo, anasema miradi ya maji inategemea malalamiko kutoka kwa jamii.

Anafafanua, licha ya kuwapo ufinyu wa bajeti isiyolingana na mahitaji, akigusia wanapatiwa bajeti ya shilingi bilioni 1.9 kwa mwaka wa fedha 2023/24 na

Inaendelea Uk. 14

AFYA

## MKAKATI KUUFUATA UMMA ULIKO...

# Anakokanyaga Samia kukabili shida afya akili, ziliko nyayo zao wananchi

- Kaunda Baraza Taifa kuwajibikia tatizo
- Staili anayozama nayo, 'PPP-matibabu'

**Na Mwandishi Wetu**

UFANISI wa jambo lolote kimantiki, hutegemea mipango na utekelezaji wake; iwe ya kijamii, kiuchumi, hata kimaendeleo.

Ndani ya eneo la afya ya umma katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambayo sasa iko mbioni kuhitimisha mwaka wa nne, suala la afya ya akili linaanzia katika udhibiti.

Msingi wake una mizizi kuanzia mipango afya, huku suala la kuimarisha afya ya akili kilishawekwa kipaumbele cha tisa, kama anavyosisitiza Meya wa Manispaa ya Songea, Michael Mbano mwezi uliopita.

Wakati kuna hayo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, akawataarifu wabunge kwamba serikali inatarajia kuanzisha Baraza la Afya ya Akili nchini.

Ni chombo kinakachosimamia muundo unaoratibu sekta za kitaaluma na kiutendaji kushughulikia ufanisi wa afya ya akili nchini.

Anarejea serikali chini ya utawala wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Afya, imekiweka kipaumbele cha tisa katika kuimarisha huduma za afya ya akili.

Ni tamko lake Majaliwa, akijibu swali la Mbunge wa Iringa, Jesca Msambatavangu, aliyedadisi uanzishaji wa baraza hilo, baada ya kukithiri matukio yasiyo ya kawaida yanayochangiwa na tatizo la afya ya akili.

Ndani yake, kuna yanayoongozwa na wizi, mauaji na mapenzi ya jinsia moja. Hapo anataja lengo ni kuhakikisha kila mwananchi, pasipo kujali mazingira yake, anapata huduma bora ya afya ya akili na kwamba huduma tembezi, ni moja ya mikakati inayolenga kufanikisha azma hiyo.




Wataalamu wakiwa pamoja kwenye kliniki ya afya ya akili, Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke, Dar es Salaam. Picha nyingine, Siku ya Afya ya Akili ilivyoadhimishwa kliniki hapo, kwa shughuli za usafi wa mazingira. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### JUHUDI MIKOANI

Kati ya Desemba 16 hadi 20 mwaka huu, mjini Songea, kulikuwapo kambi ya matibabu ya kibingwa ya afya ya akili katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Ruvuma.

"Idadi ya wagonjwa wa nje na wale wa kulazwa mnaowahudumia inaonesha kuwa hitaji la huduma hizi ni kubwa, hasa kwa magonjwa yanayoongoza kama vile msongo wa mawazo na matatizo ya utumiaji wa dawa za kulevya," anatamka Meya Mbano.

Meya huyo alimwakilisha Mkuu wa Mkoa, kwenye tukio la ufunguzi wa wiki mbili wa kambi tiba afya ya akili mkoani Ruvuma.

Anasema serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu imeweka kipaumbele kuimarisha huduma za afya ya akili akitaja lengo ni kuhakikisha kila mwananchi anpata huduma bora, pasipo kujali mazingira yake.

Anataja madaktari bingwa ya afya ya akili mkoani Ruvuma, pia wataongeza maarifa kwa watoa huduma kupitia mafunzo na kubadilishana uzoefu.

Katika hilo, Daktari Bingwa wa Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Dodoma, Dk. Sadiki Mandaru, akaitaja kambi ya pili kufanyika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. ya kwanza ilifanyika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa.

Mtaalamu huyo anataja maeneo yaliyofanyiwa uchunguzi na kupatiwa ushauri wa kisaikolojia, pia tiba ni matibabu ya sonona; wasiwasi uliopitiliza, na matumizi ya dawa za kulevya.

Ikaelezwa kuwa, madaktari hao wakatarajiwa kufanya kipimo kikubwa cha umeme wa ubongo, ambacho ni maalum kwa wenye ugonjwa wa kifafa.

Kupitia huduma hizo, ambazo mzizi wake unatokana na juhudi zake Rais Dk. Samia, Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani ya Mkoa Songea, Dk. Magafu Majura, anawashukuru ugeni huo wa kitabibu, akiutaja unasaidia kuwafikia wenye changamoto za afya ya akili.

Mnamo Oktoba 10, duniani kukiadhimishwa Siku ya Afya ya Akili, jijini Dar es Salaam katika Hospitali ya Aga Khan kulikuwapo tukio la matembezi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Gunini Kamba, akihutubia, anasema tatizo la afya ya akili ni kubwa na la muda mrefu, linalochangia kwa kiasi kikubwa na changamoto za kimaisha.

"Serikali ya Rais Dk.Samia imehimiza sana ubia na sekta binafsi hivyo kushirikiana katika matembezi haya kwa wingi ni furaha na inasaidia kufikia malengo ya kukabiliana na afya ya akili," anatamka Dk.Kamba.



Anaendelea: "Tunapoteza tukiwa kazini, tunakutana na watu tofauti tofauti na mazingira tofauti, ambayo yanaweza kupelekea tatizo la afya ya akili.

"Hivyo, ni vyema kujitambua mapema na kuchukua hatua kama mwajiri kuwasikiliza wafanyakazi wako, ili kuepukana na changamoto ya afya ya akili."

Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Afya Aga Khan, Sisawo Konteh, anashukuru jitihada zinazofanywa na wadau kukabiliana na tatizo la afya ya akili, zikiwa na msaada mkubwa kwa jamii, kukabili changamoto ya afya ya akili.

Aidha, anasema kumewekwa malengo ya kujitumia, kushirikiana na kuwa na uwazi katika kuelezea changamoto ya Afya ya akili kutawezesha elimu kufikia jamii na kuchukua hatua kupambana tatizo la afya ya akili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Marcus Mwenezi Foundation, Belinda Nyapili, anasema katika kukabiliana na changamoto ya afya ya akili, wamekuwa wakitoa elimu kwa kinamama wajasiriamali.

Ni hatua inayotajwa kufanyika katika maeneo kama vile sokoni kukabiliana na viashiria vya afya ya akili yanayoweza kuwakumba wanapokopa na biashara kutoenda vizuri.

AFYA

# Vitambue vipaumbele vitano siku zote vinavyolinda afya ya akili

Na Dk. Raymond Mgeni

MWAKA huu kwa maombi yangu, napenda ukawe unakupa fursa ya kujipa nafasi ya kujali afya ya mwili na akili kwa umma.

Huwa tunasahau sana kupanga malengo ya kiafya, pindi tunapopanga malengo ya mwaka.

Afya imebeba hatima zetu nyingi za malengo tunayoyapanga. Ikitetereka kidogo tu, hakuna kinachoweza kwenda vizuri na wakati mwingine kudorora kwa afya kunaweza kumfanya mtu kuanguka hata kiuchumi, yeye binafsi na hata jamaa zake.

Afya ya akili inabeba tafsiri kubwa ya mtu ni afya. Msingi wake ni pindi inapoguswa, basi inaangukia mtu ameguswa namna anavyofikiri, kuhisi, kutenda kwake na ufanyaji wake wa maamuzi.

Afya ya akili inapokuwa duni, inaweza kuchangia utendaji wa mtu wa kawaida ushuke, akajiumiza au kuumiza watu wengine. Hivyo inapoguswa uzito wa afya ya akili ni kuonyesha kujali umuhimu wake mkubwa kwa ufanisi wa mtu na hatimaye wa jamii inayojenga taifa.

Mwaka uliopo katika mwezi wa kwanza, zikihesabika wiki kadhaa, ni muhimu tukajenga na kuyakumbuka haya maeneo matano nitakayoenda kuyazungumzia kuyapa kipaumbele kikubwa katika hatua ya mwanzo kabisa ya kulinda afya ya akili ya mtu mzima, kwa ujumla wake.




Maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani, yaliyofanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

### USISUBIRI KUELEMEWA

Watu wengi wanaingia katika changamoto zinazohusiana na afya ya akili, kwa kuogopa kuelezea yale wanayoyapitia.

Mtu anaweza kuwa anapitia mambo mengi yanayompa mawazo au msongo mkali wa mawazo, kiasi kwamba hata utendaji wake wa mambo ni dhahiri umeshuka, si mtu wa furaha, mtu mpweke na aliyejitenga.

Hatua hizo zote kutokea, huwa kwa dharura ya mara moja. Ni vile mtu kwa muda amekuwa akipambana mwenyewe kutatua mambo ambayo hajaweza kuyapatia majibu hata hivyo.

Tumepoteza baadhi ya watu, kwa wao wenyewe kuchukua uamuzi wa kujiumiza na hata wengine kujiua, kwa kushindwa kuzungumza na watu wa karibu.

Mwaka ulipo usisubiriwe mambo yakawa magumu na yamefikia hatua mbaya, kwani ukiwa katika hatua hiyo kushughulika kwa mambo huwa ni kugumu zaidi.

Wahi mapema kusema, kuzungumza mambo yakishaanza kuonyesha hayana majibu.

### KUEPUKA UTUMIAJI VILEVI

Ni rahisi watu wengi wanapokuwa katika hali ngumu wapitiazo za msongo wa mawazo kukimbilia kutumia vilevi mfano pombe, ili kupoteza mawazo au kama njia ya kukabiliana na magumu wapitiayo.

Ubaya wa mtu aliye katika msongo mkubwa wa mawazo na vilevi ni kuwa na nafasi kubwa ya kutumia kiwango kikubwa zaidi kuliko kawaida yake.

Matumizi ya kupindukia yanaweza kuchangia zaidi matatizo kwa mtu kwa kumpa nafasi ya magonjwa ya matumizi ya vilevi, maisha kijamii kuwa na migogoro, uchumi kushuka.

Pia, ufanisi wa kazi kushuka na hata wengine kuingia katika hatari ya tabia hatarishi zinazoweza kuchangia kuingia katika ngono zembe, zinaongeza hatari ya maambukizi ya magonjwa ya zinaa, Virusi Vya Ukimwi au hata homa ya ini.

Wapo wanaotajwa kuingia kwenye vilevi kama majaribio, hususani kundi la vijana wadogo baada ya balehe.

Wengine ndio mwanya wa kujikuta tabia hiyo inakuwa endelevu na yenye kuleta madhara hapo baadaye.



Mtaalamu wa afya ya akili, Dk. Raymond Mgeni.

Jitahidi kama unaweza kuacha, kutoingia au kuepuka matumizi yoyote ya vilevi maana hatari ya matumizi ya vilevi yaweza kuleta uraibu na uraibu wa tabia.

### ANAYEWEZA KUZUNGUMZA APITIAYO

Maisha yanajumuisha watu wanaokuzunguka. Ni rahisi kwa wengine wanapopitia magumu wakajikuta wamejitenga kwa kupambana wakiwa peke yao, kuhusu magumu wapitiayo.

Huenda zipo sababu kadha wa kadha, zinazochangia watu wasipende kuzungumza magumu yao.

Moja ya sababu, niliwahi kuhoji katika semina niliyoendesha, mshiriki mmojawapo akawa na majibu:

"Tunaogopa kuzungumza yale tupitiayo, kwa sababu wengine baada ya kutusaidia wao wataanza kututangaza."

Hapo inapatikana sababu za msingi kwa watu kuogopa kuzungumza. Ikiwa una mtu anayeminiwa, basi haipaswi kungoja mambo magumu kummaliza.

Cha muhimu kinachosisitizwa hapo ni kuchukuliwa hatua ya kuzungumza au kama hakuna imani, wapo wataalamu wa afya ya akili au viongozi wa kiroho wana nafasi yao.

Kwa ujumla wake, suala la kuzungumza linapunguza uchungu na mzigo mzito mtu anaobeba ndani yake.

### MSAADA NI UDHAIFU?

Kuomba msaada pale unapokuwa na mambo mengi kichwani au moyoni, si ishara wewe ni dhaifu. La hasha! Ni kukubali jambo hilo mwenyewe umeshindwa kukabiliana nalo.

Kuhitaji msaada ni hatua ya kuonyesha ubinadamu wetu kuwa hatutaweza kuyatatua mambo yote sisi wenyewe.

Omba msaada unapoona huoni njia, huoni mwanga, huoni pa kutokea, umejaa uchungu, maumivu na hasira.

Omba msaada wakati wowote ambao unaona binafsi umefikia njiapanda. Omba msaada kwa kushirikisha kile unachopitia, ili watu wengine kama ni wataalamu au ni watu waweze kukusaidia kwa namna mbalimbali unavyoweza kutoka au kuvuka.

Usikomae mwenyewe kuonesha wewe ni jasiri sana na huombi msaada wakati mambo yako wazi umetingwa mno na njia mbele yako ina kiza kizito.

### USIJITENGE, BALI JITAHIDI

Popote maishani inatajwa ni muhimu kuwa sehemu ya jamii inayozunguka. Hao ni watu wenye msaada unaotosha wakati wowote ule unapojikuta katika hali ngumu.

Lingine ni kujenga ushirikiano mzuri na watu kila sehemu iendayo, mtu akijichanganya nao, kujenga urafiki, kushiriki kazi mbalimbali za jamii na wanajamii waweze kuona mchango wako wowote ule.

Hilo limeonyeshwa katika utafiti, kuwapo watu wanaojichanganya na kuwa karibu na jamii, ni namna moja ya kujikuta wapo katika mfumo unaowalinda kupata msaada au kutambulika haraka zaidi pindi wanapokuwa wanapitia wakati mgumu na kupata msaada, mbali na

na wale wanaojitenga wakawa na maisha ya pekee, pasipo kuchangamana.

Nikikutakia heri ya mwaka 2025, ukawe na ya kuyakumbuka, ikiwa moja ya misingi ya kuilinda afya binafsi ya akili, yakiwa salama wakati wote.

Afya ya akili kwanza, ni msingi wa jamii salama, utendaji na isiyoona haya kuzungumza mambo yote yahusuyo afya ya akili.

• ***Dk. Raymond Mgeni; ni mtaalamu wa afya na magonjwa ya akili. Kwa sasa anasoma stadi hiyo kwa ngazi ya ubingwa, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Shirikishi Muhimbili (MUHAS). Anapatikana kwa simu: +255 676 559 211***

1. 2. ends

AFYA

## KATIKA MAENEO MATANO HATARI KITAIFA...

# Manispaa Kinondoni yaanza kampeni dawa matende, mabusha kila nyumba

•Kata hatari: Tandale, M'nyamala, Makumbusho, Magomeni, Kigogo...

**Na Pilly Kigome**

HALMASHAURI ya Manispaaa ya Kinondoni, kitaifa iko katika manispaa tano nchini zinazosumbuliwa na maambukizi ya magonjwa ya matende na mabusha, ikiwagusa wanaume na wanawake kwa namna mbalimbali.

Ni jambo linaloifanya serikali kukosa usingizi kuondoa shida hiyo ndani ya manispaa hiyo.

Katika kata 20 zilizopo humo, takwimu na tafiti zinasema Kata 10 ndio zinaonekana korofi kwa kuonekana bado kuna wagonjwa na maambukizi ya maradhi hayo.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Dk.Peter Nsanya, anazitaja kata hizo ni: Kigogo, Mzimuni, Magomeni, Ndugumbi, Tandale, Kijitonyama, Kinondoni, Hananasifu, Mwananyamala na Makumbusho.

Kwa mujibu wa mganga huyo, katika kata hizo, Tandale inatajwa kuwa kinara wao, ikiwa na maambukizi ya asilimia 2.3, ikilinganisha na zingine.

Hivyo mpango uliopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, inataja kuwa na mpango kabambe wa kuondoa magonjwa hayo, ikiamini yanazuilika.

Hatua mojawapo, wamekuja na kampeni ya ugawaji kingatiba, ulioanza jana na kumalizika tarehe 26, Jumapili ijayo mchakato utakaozifikia kata hizo 10, ili kuendana na kasi ya kukabiliana na magonjwa hayo.

Dk.Nsanya anasema, katika hilo wanatarajia kuwafikia wananchi wapatao 284,036 ambao walengwa ni wananchi wote kuanzia miaka mitano na kuendelea.

Imeelezwa kuwa ni kampeni itakayofanyika 'nyumba kwa nyumba'; kwenye mikusanyiko; shuleni; vituo vya usafiri, masoko pamoja na kwenye vituo vya kutoa huduma za afya, mtazamo ni kuwafikia watu wote.



Kampeni ya kuzuia magonjwa ya matende na mabusha iliyoanza juzi kwa ugawaji dawa 'nyumba kwa nyumba' katika Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Kwa mujibu wa uongozi wa Manispaa, kumeelekezwa dira mbali inayotoa mafunzo kwa viongozi wa dini, kuhamasisha na kuwaeleza ukweli wananchi hao wajitokeze na kuacha dhana potofu kuhusiana na kinga hiyo, wakimeza dawa pasipo shaka yoyote kujihami na madhara hayo.

Shekhe Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Mohamed Muhenga anaipongeza serikali, kwa kuwapatia mafunzo na mwongozo kuhusiana na kinga hiyo.

Aidha, akaahidi kwenda kuhamasisha zoezi hilo katika nyumba za ibada ili kuweza kutokomeza maradhi hayo ambayo yanaepukika.

Mkuu wa Kanisa la Tanzania Methodist, Askofu Alex Siso anasema, wako bega kwa bega na serikali kutokomeza ugonjwa huo ambao ni wa aibu katika jamii atatumia hekima ya hali ya juu kuihamasisha jamii kumeza dawa ili kutokomeza maradhi hayo ndani ya manispaa hiyo.

Ni juhudi inayojumisha watu wa kada zote, 'watoto kwa wakubwa' kuanzia umri wa miaka mitano na kuendelea.

Rai yake kwa umma, ni kuutaka umma kujitokeze kuchangamkia fursa hiyo ya manispaa, wakiacha dhana potofu kwa baadhi ya wananchi wanaohusisha dawa hizo tafsiri inayoenezwa na baadhi ya watu "kuzuia kuzaliana", akikemea "jambo ambalo halina ukweli wowote."

Mratibu wa Miradi ya kuondoa Magonjwa ya Matende na Mabusha kutoka Ofisi ya Mkoa Dar es Salaam, Alex Mkamba, akisema jukumu ya ugawaji kinga tiba iliyoanza mwaka 2019.

Ni maeneo yenye maambukizi na ikitajwa zimesaidia kupunguza maambukizi katika baadhi ya halmashauri, ikiwa na ufafanuzi kwamba mtumiaji anaweza kumeza kabla au baada ya kula.

Mbali na Kinondoni, halmashauri zingine ambazo zina maambukizi hayo na zitafikiwa kupatiwa kingatiba ni: Mtwara Mikindani; Lindi Manispaa; Mtama mkoani Lindi; na Pangani, Tanga.

Kwa niaba ya Manispaa ya Kinondoni na serikali, shime imetolewa na kuwataka wakazi wa maeneo hayo kunywa dawa pasipo woga.

Inatajwa ni dawa salama za wananchi kuacha kupotoshana na wazazi wasiwakataze watoto wao katika unywaji dawa, ili kujikomboa, pia kujikinga na maradhi hayo.

Wanawake nao ni kundi lililotakiwa kuchangamkia fursa hiyo kwani maradhi hayo hayachagui jinsia, kwani kwa maradhi ya matende yanawakumba jinsia zote, hivyo wakatakiwa kuchangamkia zoezi hilo.

Baadhi ya maeneo ambayo yamefanikiwa katika kampeni kama hizo za Manispaa ya Kinondoni, ni wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, kulikoshuhudiwa mabadilikio kihistoria.

# Uchache vyanzo maji, shida usimamizi unavyoacha rehani afya za wanavijiji

**Inatoka Uk. 11**

bilioni 2.4 kwa mwaka 2024/25 zinazotumika kutoa huduma ya usambazaji maji wilayani humo.

Anasema, changamoto kubwa iliyopo katika maeneo mengi ni uharibifu wa vyanzo vya maji, kutokana na shughuli za kibinadamu.

**NINI KIFANYIKE?**

Hali ya ukosefu wa majisafi Msowero inafafanuliwa kuwa kielelezo cha changamoto kubwa katika utekelezaji wa Sera ya Maji ya Mwaka 2002.

Ili kufanikisha malengo ya sera hii, serikali inapaswa mambo kadhaa:

Mosi, ni kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya majisafi, hasa maeneo ya vijijini.

Pili, inatajwa kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutumia majisafi na salama.

Tatu, inagusa haja ya kupanua ushirikiano na mashirika ya misaada ya kimataifa, katika kuongeza vituo vya maji.

Pia, kuna hoja inayoangukia serikali na wadau wengine wanapaswa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha wakazi wa Msowero wanapata huduma hiyo muhimu.

Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, inaorodhesha malengo makuu matatu, inayoandaa mfumo unaokuza maendeleo bora, endelevu na sawa ya rasilimali za maji kwa manufaa ya Watanzania wote.

Pia, suala kuboresha afya na kupunguza umaskini wa wakazi vijijini, kwa kuboresha upatikanaji huduma za maji.

Ripoti za mwaka jana, za Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF) zinaeleza kiasi kikubwa, kuwa mabilioni ya watu duniani wanaendelea kutaabika kutokana na kukosa huduma bora za maji na masuala ya usafi.

Hata hivyo ripoti hiyo inasema takribani watu bilioni 2.2 duniani kote, hawana huduma ya maji safi na salama ya kunywa.

Vilevile, kuna watu bilioni 4.2 hawana huduma salama za usafi na watu bilioni tatu wanakosa huduma za msingi kwenye sehemu za kunawa mikono.



# DC mbogo vyanzo vya maji kukauka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani hapa, Simon Mayeka amewaamuru viongozi wa Kata ya Ng'humbi kuhakikisha watu waliovamia Hifadhi Misitu ya Mazingira wanarejesha vyanzo vya maji vilivyokauka kwa maslahi ya taifa na wananchi.

Vilevile, Mayeka ameuamuru uongozi wa vijiji vya Ng'humbi na Mbagilwa wilayani humo kuwasilisha majina ya watu hao ofisini kwake ili wachukuliwe hatua kwa kosa la kuharibu mazingira ya hifadhi hiyo na kuvamia vyanzo hivyo vya maji.

**Naomba viongozi wa kata hii na vijiji kwa kushirikiana na wilaya simamieni maagizo yaliyotolewa kuhusu utunzaji mazingira hatuhitaji kuona wavamizi kwani wanaharibu vyanzo vya maji na misitu.**

Mayeka alitoa amri hiyo juzi wakati wa ziara yake na wataalam wa mazingira kwenye safu ya milima ya Tangalata ya hifadhi hiyo iliyopo mpakani mwa Kijiji cha Mbagilwa cha Kata hiyo.

Alisema viongozi wa vijiji hivyo wanapaswa kuzuia wa shughuli za kibinadamu zilizopigwa marufuku na serikali katika maeneo ya hifadhi hiyo ili kudhibiti uharibifu wa mazingira unaoendelea katika milima hiyo na kunusuru vyanzo vya maji.

"Naomba viongozi wa kata hii na vijiji kwa kushirikiana na wilaya simamieni maagizo yaliyotolewa kuhusu utunzaji mazingira hatuhitaji kuona wavamizi kwani wanaharibu vyanzo vya maji na misitu," alisema Mayeka.

Alimuagiza Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Kongwa kuweka doria kuhakikisha hakuna mtu anayevamia na kufanya shughuli yoyote katika milima hiyo.

Alisisitiza kuwa mazao yote yaliyopandwa katika milima hiyo yasiguswe wala kuendelezwa bila kibali maalum kutoka ofisini kwake.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Farouk Isa, alisema wavamizi wa milima hiyo wanatoka Kijiji cha Mbagilwa.

Isa, alisema aliomba nguvu za kiusalama kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kudhibiti uharibifu huo kutokana na mazingira magumu ya eneo hilo.

Alisema wavamizi hao wanajulikana na wamekuwa wakikaidi kutekeleza maagizo ya serikali ngazi ya kata ili kuhifadhi mazingira na kusababisha vyanzo hivyo vya maji kukauka.

Akizunguza wakati wa ziara hiyo, Ofisa wa TFS wa Wilaya hiyo, Patrick Mbughi, alisema milima hiyo ina vyanzo vya maji vitatu, baadhi vimekauka kutokana na uvamizi huo na madaraja katika Kijiji cha Ng'humbi kusombwa na maji.

Mbughi, alifafanua madaraja hayo na baadhi ya miundombinu inayotumiwa na wananchi, vimesombwa na kasi kubwa ya maji kutoka milimani kushuka kwa wingi.

# Halmashauri yataja vipaumbele 2025/26

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Singida inatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 45.2 kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 kuboresha huduma za jamii, kutekeleza miradi ya maendeleo na kulipa stahiki wafanyakazi wake.

Mpango huo ulitangazwa mwanzoni mwa wiki hii na Mchumi wa Halmashauri hiyo, Jeremiah Kikonge wakati akiwasilisha bajeti kwa mwaka huo kwenye Kikao cha Baraza la Wafanyakazi.

Kikonge, alisema halmashauri hiyo inatarajia kukusanya fedha hizo kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya matumizi hayo.

"Bajeti ya 2025/2026 tumeweka vipaumbele vya ukamilishaji miradi ya viporo, huduma za jamii za afya, elimu, na masuala ya mtambuka. Kuanzisha miradi ya kimkakati na kukamilisha jengo la utawala la halmsahuri, " alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Joanfaith Kataraia, alisema katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa umma, watahakikisha wainaimarisha ushirikiano baina yao.

Joanfaith, alisema ushirikiano huo utasaidia kutatua changamoto zinazojitokeza kati ya mwajiri na mwajiriwa na kuleta tija na utoaji huduma sawa kwa wananchi.

Alisema hatua hizo mpya hazilengi tu kuboresha mazingira ya kazi, bali pia kuinua kiwango cha utoaji huduma kwa wakazi wa halmashauri hiyo na kuondoa malalamiko miongoni mwao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mkoa wa Singida, Hamisi Mtundua, aliipongeza halmashauri hiyo kwa bajeti hiyo na kuomba ikafanye kazi iliyokusudiwa, ikiwemo stahiki zote za watumishi na kuwa chachu ya kuwaletea wananchi maendeleo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Justin Nyamoga (kushoto), akizungumza wakati akiongoza kikao walipokutana na Uongozi wa Wizara hiyo, jijini Dodoma jana. Wa pili kulia ni Waziri wa TAMISEMI, Mohamedi Mchengerwa na kulia ni Naibu wake, Zainabu Katimba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Madaktari wanolewa tiba afya ya akili

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WIZARA ya Afya kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ya mkoani hapa, imetoa mafunzo maalumu kwa madaktari wa hospitali za rufaa za mikoa nchini kwa lengo la kuboresha huduma za afya ya akili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala aliyasema hayo mwanzoni mwa wiki hii wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo ya siku tano kwa madaktari hao.

Dk. Lawala, alisema mafunzo hayo yatasaidia jamii kuepukana na magonjwa ya afya ya akili.

Alitoa rai kwa wataalum wa afya ya akili kuwa mabalozi wa taaluma yao ili kuikuza kwa kuchukua hatua za haraka kuwa madktari bingwa wa afya hiyo.

"Ukishauelewa ubongo wa binadamu umeielewa dunia yote na utakuwa mtu muhimu katika jamii na taifa kusaidia taifa kupigana na magonjwa ya afya ya akili", alisisitiza Dk. Lawala.

Alizipongeza hospitali hizo za mikoa ya Iringa na Njombe kwa kuanza kutoa huduma za afya ya akili zilizokamilika.

Alisisitiza hospitali hizo kupewa nguvu na uongozi ili kutoa huduma zilizokamilika kwa kuona na kulaza wagonjwa na kupunguza rufaa zisizo za msingi za wagonjwa wa afya ya akili.

# TRA yapewa somo kuondoa malumbano kudai kodi

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetakiwa kutoa elimu ya aina ya kodi wanazopaswa kutoa wawekezaji kabla ya kuanza kufanya biashara ili kuepuka malumbano baina yao na maafisa wake.

Rai hiyo imetolewa na Mwakilishi wa Wazalishaji wa Mvinyo wa Kampuni ya CETAWICO ya jijini Dodoma, Catherine Mwembe wakati akitoa maoni kuhusu kuboreshwa kwa mfumo wa ulipaji Kodi nchini.

Maoni hayo alitoa juzi katika kikao baina ya walipakodi na Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi nchini inayoongozwa na Balozi Ombeni Sefue.

Catherine, alisema wawekezaji nchini wanatakiwa kuelimishwa aina ya kodi wanapaswa kulipa kwenye biashara zao nchini ili kuepusha malumbano hayo, baadhi kufunga biashara na kuwakimbia maafisa hao.

Alilalamikia utitiri wa kodi kwa madai umekuwa kero kwa walipakodi na chanzo cha wengi wao kukwepa kulipa kwa kufunga biashara na kuwakimbia maofisa hao wanapofika kwenye biashara zao.



# Watangaziwa fursa hewa ya ukaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI mkoani hapa wamehamasishwa kuchangamkia fursa ya kupanda miti kwa wingi ili kufikia soko la kimataifa la uvunaji wa hewa ukaa na kukuza uchumi wao.

**Fursa hiyo inaweza kuwa na uwezo wa kubadilisha hali ya uchumi kwa mkulima mjini Njombe.**

Wito huo ulitolewa juzi na Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Maxon Msigala wakati wa kampeni ya upandaji miti katika eneo oevu la Lunyanywi ili kukabiliana mabadiliko ya tabia ya nchi lililoratibiwa na Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Mkoa wa Njombe.

Msigala, alisema kwa sasa hewa ya ukaa ipo sokoni, hivyo wananchi wakipanda miti ya kutosha na kuuza kwa kampuni za baadhi ya mataifa duniani ikiwemo Marekani.

"Kwa maana wanaangalia kiwango cha mti kilichopo na wanathaminisha na kiwango cha hewa ya ukaa kinachopatikana pale, hivyo mnakuwa mnalipwa fedha," alisema Msigala.

Alisema fursa hiyo inaweza kuwa na uwezo wa kubadilisha hali ya uchumi kwa mkulima mjini Njombe.

"Nawahimiza kushiriki kwa wingi ili kuhakikisha mnakumbatia maendeleo yanayoendana na mahitaji ya dunia kwa sasa," alisema Msigala.

Kwa upande wao wanachama hao, akiwemo Esther Mtanga alisema kwa kushirikina na maofisa wa maliasili wamepanda miti zaidi ya 100 ikiwa ni kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kuteuliwa kuwa mgombea urais katika Uchaguzi Mkuu mwaka huu kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Katibu wa Chama hicho, Saada Msangi, alisema wanatuma salamu za pongezi kwa Rais Samia kwa kupanda miti ili kumuunga mkono kwenye mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira.

Fursa ya kupanda miti kwa ajili ya soko la hewa ukaa ni hatua muhimu ya kiuchumi na kimazingira katika mkoa wa Njombe.



Koplo Gladness Sizya wa Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe, akizungumza na wanafunzi wa kidato cha kwanza wa Shule ya Sekondari Nsenya jana, baada ya kuwapa elimu ya madhara ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto ikiwa ni mwendelezo wa Kampeni ya "Tuwaambie kabla hawajaharibiwa".
**PICHA: ISSA MWADANGALA**

# Polisi wanasa madereva 5,900 barabarani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la polisi Mkoa wa Njombe limewashikilia zaidi ya madereva 5,900 kwa tuhuma za kukiuka sheria za usalama barabarani na kumfungia leseni mmoja.

Hayo yalisemwa juzi na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Mahamoud Banga wakati akitoa taarifa ya mwezi mmoja kwa waandishi wa habari za matukio ya uhalifu mkoani hapa.

Banga, alisema kati ya madereva hao waliokamatwa 5,929, walioandikiwa faini ni 5,927.

Alisema madereva hao walikamatwa kufuatia oparesheni iliyofanywa na jeshi hilo katika maeneo mbalimbali mkoani hapa ili kudhibiti ajali za barabani.

Alitoa wito kwa wakazi wa Njombe kuacha tabia ya kuhujumu miundombinu ya nchi ikiwemo ya maji na kukemea vitendo vya ukatili kwa tamaa ya kupata mali kwa haraka hali inayosababisha baadhi yao kujiingiza katika uhalifu.

# Wazazi watakiwa kupinga udhalilishaji watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZAZI na walezi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani hapa Mkoa wa Njombe, wametakiwa kushirikiana katika malezi na kupinga udhalilishaji watoto ili kuwaepusha na athari za kisaikolojia na kimwili.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi wa Halmashauri hiyo, Samwel Kombe wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwitikio wa wazazi kuandikisha watoto wao kujiunga na elimu ya awali na msingi.

Kombe, alisema jamii bado inatakiwa kukabiliana na vitendo hivyo vikiwemo vya ubakaji na ulawiti kwa watoto wadogo kwa kuwa vinawaathiri kiakili.

"Bado tunachangamoto ya vitendo vya udhalilishaji katika mji wetu wa Makambako, nawaomba sana wazazi, jamii na walezi hali inatisha watoto hawa watakosa amani, tusaidiane kuvipunguza vitendo hivi," alisema.

Alisema hadi sasa wamefikia malengo ya kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza kwa asilimia 100.3 na la awali asilimi 70.1 na kushindwa kufikia malengo kwa kundi hilo.

Baadhi ya wazazi mjini huko, walisema changamoto kubwa inayosababisha washindwe kuwapeleka watoto kujiunga na dasara la awali ni wengi wao kuwapeleka watoto wao kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

"Tunaiomba serikali wote wanaotuhumiwa na kesi za ukatili wachukuliwa hatua za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo," alisema Sanga.



## Wizara zashauriwa kushirikisha maofisa habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa wizara na taasisi za serikali visiwani hapa wameshauriwa kuwashirikisha maofisa habari na katika mijadala, makongamano na maonesho ili kuleta ufanisi zaidi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maofisa Habari na Uhusiano wa Serikali Zanzibar (ZICOO), Raya Hamad Suleiman, alitoa ushauri huo wakati akizungumza na Nipashe visiwani hapa. Suleiman, alisema ametoa rai hiyo kutokana na maofisa hao kuwa kiungo kuhamasisha wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya taasisi na wizara hizo.

Alisema maofisa hao wanasaidia kuimarisha mahusiano kwa kuwasikiliza wananchi, kujibu maswali yao na kupokea maoni.

" Kushirikisha vitengo vya habari vya kila idara na taasisi ni muhimu kufanikisha matukio ya kitaifa," alisisitiza Mohamed.

Alisema ni jambo jema maofisa hao wameshikiri kikamilifu kuandaa kazi za taasisi na wizara zao ikiwemo taarifa za utekelezaji, mafanikio, vipaumbele na mwelekeo.

Akizungumzia maonesho ya biashara yaliyofanyika viwanja vya Nyamanzi na Chamanangwe Pemba hivi karibuni, aliwapongeza maofisa hao kwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu ikiwemo kutoa elimu kwa wananchi.

"Jambo hili limefanikiwa kwa asilimia kubwa kwani wananchi waliotembelea mabanda ya maonesho wamenufaika na elimu, kufahamu majukumu na kutangaza mafanikio ya wizara na taasisi zote za serikali yetu na wengine kupata huduma za papo kwa papo ikiwemo kupata vitambulisho," alisema Mohamed.

Alitumia nafasi hiyo kuipongeza Idara ya Habari (MAELEZO) Zanzibar kwa kusimamia taarifa za mafanikio ya wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na kutangazwa kwenye vyombo vya habari.

# SMZ yajivunia watalii kumiminika Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar (SMZ) imesema inaona fahari kwa mafanikio inayoendelea kupata katika Sekta ya Utalii kutokana na wageni kuzidi kumiminika kutembeleza vivutio vilivyopo visiwa vya Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga wakati akizungumza na wadau wa utalii visiwani hapa, taasisi na kampuni zinazopokea na kutembeza watalii.

Soraga, alisema wageni hao wakiwemo watu maarufu kutoka sehemu mbalimbali duniani, wanamiminika kutembelea vivutio vya utalii kutokana na amani na utulivu visiwani hapa.

Alisisitiza kuwa ni jukumu la kila mmoja kuwa mlinzi wa amani hiyo iliyopo nchini ili idumu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Alisema serikali inaona fahari kwa watalii wengi kuchagua Zanzibar kwa amani iliyopo kuwahakikishia mapumziko na matembezi ya furaha na kusababisha sekta ya utalii haiyumbi.

Pamoja na mambo mengine, Soroga, alisema kufanikiwa kwa maonesho ya kwanza ya utalii na uwekezaji yaliyofanyika Oktoba mwaka jana katika Viwanja vya Nyamanzi ni matunda ya amani na utulivu visiwani humo.

Hata hivyo, alisema kibinadamu wakati mwingine kunaweza kutokea vitendo vichache vya uvunjifu wa amani hata katika maeneo ya utalii mbele ya wageni na kusisitiza vyombo vya dola na kamati za ulinzi za mikoa na wilaya viko makini kudhibiti.

"Kwa mfano sisi wizara pamoja na Kamisheni ya Utalii hatukufurahishwa na tukio la watembeza watalii na askari waliokuwa wakitekeleza majukumu yao katika eneo la hifadhi bahari ya Fumba. Tunashukuru vyombo vya dola vilichukua hatua, nasi tulifanya vikao kadhaa kuelekeza miongozo inayofaa na tumefahamika," alifafanua.

Alisema kuelekea maonesho ya pili ya mwaka huu yatakayofanyika mwishoni mwa mwezi Mei badala ya Oktoba, wananchi wanapaswa kuendelea kutunza amani na kuonesha ukarimu ili Zanzibar ibaki kuwa kivutio na kituo kikuu cha kutembelewa na watalii wa viongozi wa mataifa mbalimbali duniani.

"Sote tunajua amani ni tunu isiyofaa kujaribiwa kwani ikitoweka hakuna kiasi chochote cha fedha kinachoweza kuinunua. Yamkini kuipoteza iwe rahisi, lakini ugumu uko katika kuirejesha tena. Tutimize wajibu wetu kuidumisha kwa maslahi yetu kiuchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa letu," alisema Soroga.

Mkurugenzi Masoko Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahma Sanya, alisema tamasha hilo la pili la utalii na uwekezaji litakuwa la kuvutia zaidi kutokana na maandalizi yake.

Rahma, ambaye pia ni Kaimu Katibu Mtendaji wa kamisheni hiyo, alisema Juni mwaka huu kwa mara ya kwanza Zanzibar itakuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa mashirika ya usafiri wa anga barani Afrika.

Alisema mkutano huo utahudhuriwa na watu 500 na kukutanisha mashirika yote ya ndege duniani.

Alisema mkutano huo utakuwa na umuhimu mkubwa katika azma ya Zanzibar kuimarisha utalii wake, kushawishi mashirika mengi zaidi ya ndege kuanzisha safari zake visiwani hapa.




Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Zanzibar, Abeida Rashid Abdallah (kushoto) na Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Arusha, Dk. Bakari George, wakibadilisha hati mjini Zanzibar juzi, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano wa kubadilishana uzoefu kwa lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanachama CCM zaidi kujiandikisha kupiga kura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANACHAMA wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Kisiwa cha Unguja wamesema watajiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya kushiriki Uchaguzi Mkuu mwishoni mwa mwaka huu.

Wakizungumza kwa nyakati na gazeti hilo, walisema kujiandikisha kwao katika daftari hilo kutaongeza wingi wa kura katika uchaguzi huo wa rais, wabunge na wawakilishi na kutimiza matakwa ya chama hicho ya kushika dola baada ya kupata ushindi wa kishindo.

Kauli ya wanachama hao imekuja kufuatia Mkutano wa CCM kumpitisha Mwenyekiti wa chama hicho taifa ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa wagombea urais katika uchaguzi huo.

Ibrahim Makame Juma, Mkazi wa Amani, alisema viongozi hao wana maono ya kuleta maendeleo kwa taifa.

Juma, alisema viongozi hao watakaposhika madaraka kwa awamu ya pili, watatimiza ndoto zao za kumaliza ahadi na kujenga nchi kwa kutumia falsafa ya uchumi kama walivyoanza katika kipindi cha miaka minne ya uongozi.

"Tutajiandikisha ili kuongeza idadi ya kura kwa viongozi wetu na kuona wanashinda kwa kishindo kwenye Uchaguzi wa 2025," alisema.

Fahad Ali Mohamed, Mkazi wa Kikwajuni, alisema viongozi hao watakapopewa nafasi kwa awamu nyingine, watajenga miundombinu imara na kuwa mfano kwa mataifa mengine duniani.

"Ukifika Tanzania au katika visiwa vya Zanzibar utaona maendeleo makubwa yamefikiwa kwenye ujenzi wa nyumba za makaazi, barabara za ndani vijijini na mijini, usafiri wa anga na nchi kavu," alisema Mohamed.

Hassan Nassir Suleimana, Mkazi wa Michenzani, alisema tangu viongozi hao washike madaraka, nafasi za ajira kwa vijana zimeongezeka.

Wakati huo huo; Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Wilaya ya Kaskazini 'A', Ashura Abdi Fom amewapongeza wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho kwa kuifanyia maboresho katiba ya chama chao na kutoa miongozo ya usimamizi na utekelezaji wa chama.



Mwenyekiti Mpya wa Chadema Taifa, Tundu Lissu

MIONGO MIWILI UBIA NA MBOWE

# Kutoka gerezani hadi Mwenyekiti CHADEMA

**Na Sabato Kasika**

MWANASIASA Tundu Lissu amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), baada ya mchuano mkali kati yake na aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Freeman Mbowe.

Wakati Lissu amechaguliwa kushika nafasi hiyo, ni vyema Watanzania wamfahamu kuwa ni nani katika harakati za kisiasa hadi kufikia katika nafasi hiyo.

Awali, Lissu alikuwa mwanachama wa chama cha NCCR- Mageuzi kabla ya kujiunga na CHADEMA mwaka 2004 baada ya Mbowe kuvutiwa na harakati zake za kutetea watu na kumwomba waungane.

Ilikuwa mwaka 2003 wakati mwanasiasa huyo akifuatilia kesi za wananchi wa Nyamongo, Tarime mkoani Mara, waliokuwa wamewekwa gerezani, huku diwani wa CHADEMA, Chacha Wangwe (marehemu), akikabiliwa na kesi 10 za jinai.

Katika harakati hizo, hata yeye Lissu aliwekwa ndani lakini hakuchoka kuendeleza harakati zake za kuwatetea wananchi dhidi ya wawekezaji. Ndiye aliyewatoa bure gerezani wananchi 446 wa Nyamongo Tarime.

Wananchi hao waliwekwa gerezani kwa kupinga kunyanyang'anywa ardhi yao na mwekezaji, kitendo kilichomfanya azidi kuwa maarufu katika harakati zake za kutaka haki ipewe nafasi.

Harakati zake hizo zilimfanya ajulikane kutokana na kuandikwa mara kwa mara kwenye vyombo vya Habari, hivyo kujiongezea umaarufu na kuwavutia wanaharakati wengi, wakiwamo walio katika vyama vya siasa.

Wakati akifanya harakati hizo, akiwa mwanachama wa NCCR- Mageuzi. Mbowe hakujua hilo. Alidhani ni wa CHADEMA, hivyo akamwomba atafute wanaharakati wengine awapeleke CHADEMA.

Mbowe aliamini kuwa Lissu ni mwanachama wao kwa kuwa anafanya harakati ambazo wao CHADEMA walikuwa wakizifanya. Lissu aliamua kubadili gia angani na kujiunga na CHADEMA mwaka 2004.

Hivyo ndivyo mwanasiasa huyo alivyojiunga na CHADEMA na amekuwa akijitanabahisha ndani na nje ya chama chake kuwa ni mwenye msimamo usiyeyumba wala hataki kuona mtu akionewa.

Ni Lissu huyo ambaye aliyewahi kuwekwa ndani na kupigwa marufuku kufika Nyamongo. Ni yeye aliyepambana na serikali ya Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, ili isiuze Rufiji Delta kwa mwekezaji mmoja hadi benki nazo zikaacha kutoa mkopo kwa mwekezaji huo.

Pia ni Lissu huyo huyo aliyeanza kushtakiwa kwa uchochezi mwaka 2001. Katika kesi nyingi anazozisimamia, huwa halipwi na watu anaowatetea, bali hufurahi anapoona mtu haonewi au kunyanyaswa.

**UANAHARAKATI**

Historia inaonesha kuwa tangu akiwa shule ya msingi, alionesha kuwa mwanaharakati. Alikuwa akikataa kuona wanafunzi wanawachotea maji walimu, kulima mashamba ya walimu na kupanda mazao. Alikuwa akiona kuwa utaratibu huo hauko sawa.

Utaratibu mwingine ambao alikuwa akiupinga ni kuamka alfajiri saa 11:00 ili saa 12:00 kuwa shuleni na kwamba alikuwa muasi na alibishana na walimu kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu.

Historia pia inaonesha kuwa alizaliwa katika familia ambayo mijadala ya kisiasa ilikuwa ya kawaida na kwamba baba yao alisoma hadi darasa la sita.

Katika maisha yao, kila siku jioni walikuwa wanasikiliza kwanza taarifa ya habari na Idhaa ya Kiswahili ya Ujerumani, kisha mjadala wa kisiasa kuhusu mwenendo wa mambo ya dunia hadi hadi saa 5;00 au 6:00 usiku.

Akiwa darasa la kwanza mwaka 1976, alikuwa anafahamu karibu viongozi wote duniani na miji mikuu mashuhuri.

Wakati akiwa sekondari, historia inaonesha kuwa amewahi kutuhumiwa kuleta uchochezi, akasimamishwa shule kutokana na harakati za kutetea haki, akawa amerudishwa shuleni.

# Wachambuzi waona nuru mpya CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kupata viongozi wapya, wachambuzi wa masuala ya siasa wamesema hatua hiyo itakiimarisha chama na kuwa imara zaidi.

Wamesema CHADEMA imeonyesha ukomavu wa kisiasa ambao unapaswa kuigwa na vyama vingine vya siasa ndani na nje ya nchi.

Wakizungumza na Nipashe, wachambuzi hao pia walisema kupatikana kwa uongozi mpya baada ya miaka 20, kutaleta ushindani katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji Mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo-Bisimba, alisema kupatikana kwa viongozi wapya wa CHADEMA kwa njia ya kikatiba ni ukomavu wa kisiasa unaopaswa kuigwa na vyama vingine nchini.

"Watu kwenye uchaguzi wa chama chao wameamua kufanya uchaguzi kisheria. Amepatikana mshindi lakini nilichofurahi aliyeshindwa amekubali. Hii wamefundisha maana ya demokrasia.

"Wengine kwa uchaguzi kama huo utakuta wanazinguana, wanahama. Ni dalili nzuri kama watashikamana na kuendelea vizuri," alisema.

Dk. Kijo-Bisimba alisema tangu awali alitoa maoni kwamba kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi, tofauti za ndani ya chama ziwekwe kando ili kutoa fursa ya mshikamano.

Alisema huu ni mwaka wa uchaguzi hivyo CHADEMA wanapaswa kuweka pembeni tofauti zao kwa sababu wao ndiyo chama kikuu cha upinzani.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Sabatho Nyamsenda, alisema matokeo hayo yanaashiria kuwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu Chama Cha Mapinduzi (CCM) kijiandae kupate upinzani mkubwa.

Alisema hali hiyo inatokana na mitazamo na sera alizo nazo Mwenyekiti mpya wa chama hicho, Tundu Lissu, za kuendesha siasa za kiunaharakati zinazohusu kudai mageuzi, utawala bora na kufichua ufisadi tofauti za mtangulizi wake aliyekuwa anaegemea katika maridhiano.

Nyamsenda alisema endapo Lissu ataenda na itikadi hizo katika uchaguzi huo, ana nafasi kubwa ya kuongeza idadi ya kura kwa sababu ndizo itikadi ambazo ziliwavuta wanachama wengi kabla ya Mbowe kuleta maridhiano.

Pia alisema ili chama kitekeleze yale ambayo Lissu amejinadi nayo, hakina budi kuanza kufanya mabadiliko ya ndani ili wanachama wote wasimame wakiwa na mtazamo mmoja.

Mchambuzi wa siasa na mwanadiplomasia, Hamduni Maliseli, alisema ushindi wa Lissu unaonesha mtazamo wa wanachama wa CHADEMA wa kubadilisha viongozi ili kuleta mabadiliko wanayoyakusudia.

Alisema uchaguzi huo ulivyokuwa na ushindani mkubwa hadi kusababisha matokeo yanayolingana, unaleta taswira kuwa viongozi hao wamegawana wanachama nusu kwa nusu na kukishauri chama hicho kuliangalia suala hilo kwa makini.

Aidha, aliwakumbusha Mbowe na Lissu kutekeleza kwa vitendo ahadi za kuendelea kushirikiana katika kukijenga chama hicho baada ya matokeo, ili kuleta umoja na mshikamano ndani ya chama.

Mhadhiri msaidizi kutoka Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Idara ya Habari na Ukutubi, Vincent Mpepo, alisema mchakato uliofanyika ndani ya CHADEMA wa kuwapata viongozi wa kitaifa ni salama kwa nchi za Afrika katika kuleta mabadiliko.

Mpepo alisema baada ya Lissu kutangazwa kuwa mshindi, kazi iliyobaki ni kukiimarisha chama kwa kushirikiana na wenzake badala ya kuendeleza migogoro na kutuhumiana.

Naye Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi, Dk. Joshua Mwaipape, alisema demokrasia imeshinda katika uchaguzi huo.

Alieleza kuwa wanachama na wananchi walihitaji Lissu ndiye awe kiongozi wao na ndivyo ilivyokuwa hali hiyo imeonesha kuwa demokrasia ilichukua nafasi yake kwenye mchakato wa kumpata kiongozi.

"Kilichotokea kwenye uchaguzi huu kimesababisha vijana na wanachama wawe wajasiri, angechaguliwa mwingine kungeibuka maswali mengi, kwa sababu mahitaji yao yalikuwa ni Lissu," alisema Dk. Mwaipape.

Alisema kwa matokeo hayo uhai wa CHADEMA umeongezeka na wanakwenda kuimarika zaidi.

**Imeandaliwa na Jenifer Gilla, Halfan Chusi, Christina Mwakangale, Grace Mwakalinga.**

HABARIKIMATAIFA

# Mkuu wa Majeshi Israel ajiuzulu

**TEL AVIV, Israel**

MKUU wa Jeshi la Israel, Meja Jenerali Herzi Halevi, amejiuzulu nafasi yake kutokana na kushindwa kuzuia uvamizi uliofanywa na kundi la wanamgambo la Kipalestina la Hamas, Oktoba 7, 2023.

Katika barua yake ya kujiuzulu, Meja Jenerali Halevi, alitoa ufafanuzi kuhusu sababu za kujiuzulu kwake akikiri kwamba alishindwa kuzuia uvamizi huo uliofanywa ndani ya ardhi ya Israel. Alisema anaondoka kwenye nafasi hiyo wakati yamepatikana mafanikio kwa jeshi hilo katika vita vya ukanda wa Gaza.

Aidha, kiongozi wa upinzani wa Israel, Yair Lapid ameitaka serikali ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu nayo kujiuzulu baada ya mkuu huyo wa jeshi kuamua kuondoka madarakani.

Wakati huohuo, vikosi vya Israel vimeanzisha operesheni kubwa ya kijeshi katika mji unaokaliwa kwa mabavu na nchi hiyo wa Jenin, ulioko Ukingo wa Magharibi.

Wizara ya Afya ya Palestina ilisema takribani watu sita wameuawa na wengine 35 wamejeruhiwa.

*DW*



Wakazi wa mji wa Minova wakikimbia mapigano kati ya jeshi la DRC na waasi wa M23 kupitia Ziwa Kivu kutafuta hifadhi katika mji wa Goma. **PICHA: AFP**

# Trump amwonya Putin akikataa mazungumzo

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameionya Russia kuwa huenda itawekewa vikwazo, kama Rais Vladimir Putin hatakubali kufanya mazungumzo ya kumaliza vita nchini Ukraine.

Hata hivyo, Rais Trump hakutoa ufafanuzi kuhusu aina ya vikwazo hivyo vipya, ingawa tayari Marekani imeiwekea nchi hiyo vikwazo vingi kufuatia uvamizi wake katika nchi ya Ukraine Februari 2022.

Kiongozi huo pia alidokeza kwamba serikali yake inatafakari suala la kupeleka silaha kwa Ukraine na kuutaka Umoja wa Ulaya kufanya mengi zaidi kuiunga mkono nchi hiyo.

Rais Trump, alisema wako katika mawasiliano na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy na wanatarajia kuzungumza na Putin hivi karibuni.

Aidha, Trump alieleza kuwa alimuhimiza Rais wa China, Xi Jinping, kutumia ushawishi wake kumaliza vita hivyo, kutokana na taifa hilo kuwa na nguvu kubwa.

Alisema katika vita hivyo, Rais Xi hajaonyesha juhudi za kutosha kusitisha mgogoro huo.

Wakati huo huo, Rais Vladimir Putin alimwita Rais wa China Xi Jinping, kama rafiki mpendwa wakati wa mazungumzo waliyoyafanya kwa njia ya simu.

Mazungumzo hayo yaliyodumu kwa muda wa takriban saa moja na nusu yalifanyika saa chache baada ya Donald Trump kuapishwa, viongozi hao waliahidiana kujenga uhusiano imara zaidi.

Rais Xi alisema nchi yake na China zinajenga uhusiano kwa msingi wa urafiki, kuaminiana na kusaidiana licha ya kuwepo shinikizo kutoka nje.

Rais Xi alitoa wito kwa Putin kuendelea kuimarisha uratibu wa kimkakati, kuimarisha msaada wa pande zote, na kulinda maslahi halali.

Hata hivyo Rais Putin alimwambia Xi, kwamba suluhu katika vita vya Ukraine ni lazima iheshimu maslahi ya Russia kwanza.

## Afrika Kusini yarudisha usafiri wa ndege Tanzania

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

SHIRIKA la Ndege la Afrika Kusini (SAA) limezindua rasmi safari zake za kila siku kati ya majiji ya Johannesburg, na Dar es Salaam nchini Tanzania.

Hatua hiyo ilielezwa inalenga kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kati ya mataifa hayo mawili yenye ushawishi barani Afrika.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa muda wa SAA, Prof. John Lamola, alisema usafiri huo ni daraja la kuunganisha nchi hizo yenye nguvu za kiuchumi.

„Njia hii ya anga si tu hatua muhimu kwa SAA katika kuunganisha Johannesburg na Dar es Salaam, bali pia inatangaza daraja linalounganisha mataifa mawili yenye nguvu kiuchumi. Inaleta pamoja viwanda, jumuiya na rasilimali, huku ikifungua milango ya fursa mpya za biashara, uwekezaji na maendeleo kwa watu wa Afrika Kusini na Tanzania," alisema.

Alisema kuwa Dar es Salaam ni mji muhimu kimkakati Afrika Mashariki, pia ni kitovu cha kiuchumi na lango kuu la biashara na usafirishaji wa mizigo katika ukanda huo na pia kituo cha watalii wanaokwenda Hifadhi ya Serengeti, Mlima Kilimanjaro na visiwa vya Zanzibar.

Aliongeza kuwa Afrika Kusini ni mwekezaji mkubwa nchini Tanzania, hasa katika sekta za kilimo, madini, kemikali, na mashine. Alibainisha kuwa uzinduzi wa safari hizo unatarajiwa kukuza zaidi ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizi mbili.

*SAA*

## Vurugu zaleta hasara Bandari ya Maputo

**MAPUTO, Msumbiji**

MSUMBIJI imeeleza kuwa maandamano yaliyoambatana na ghasia baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana, kumesababisha bandari yake kubwa kupata hasara baada ya kushuka kwa huduma ya uchukuzi.

Maandamano hayo yalilazimisha wafanyabiashara wanaotumia bandari ya Maputo, kusitisha kuitumia kutokana na barabara kadhaa kufungwa.

Wanaendesha bandari hiyo walisema kwamba shughuli za usafirishaji mizigo kwenye bandari hiyo kwa mwaka jana zilishuka kwa asilimia moja na kufikia tani milioni 30.9 ikilinganishwa na tani milioni 31.2 zilizorekodiwa kusafirishwa 2023.

Taarifa hiyo ilisema kushuka kwa shughuli za kibiashara kumesababishwa na hatua mbali mbali na hasa kufungwa kwa mpaka na barabara kwa siku chungu nzima kutokana na maandamano yaliyosababishwa na vurugu za kisiasa.

*DW*

# SINGIDA BS YATANGAZA RASMI KUMREJESHA GADIEL LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Black Stars inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imeamua kumrejesha nchini mchezaji wake wa zamani, Gadiel Michael, ambaye alikuwa akiichezea Chippa United ya Afrika Kusini.

Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, alisema jana, wameamua kumrejesha nyota huyo ili kukiongezea nguvu kikosi chao kuelekea kuusaka ubingwa wa Ligi Kuu.

Massanza alisema timu yao inahitaji kuwa na wachezaji wenye uzoefu kwa sababu wanahitaji kufikia malengo yao ya kupata moja kati ya nafasi nne za juu, ili kukata tiketi ya kucheza mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Tumemrudisha Tanzania mchezaji katika kiwango kisichoshuka, Gadiel, tunamkaribisha nyumbani na kwenye timu yake ya zamani, naamini sasa tumekamilika na tuko tayari kwa mapambano ya mzunguko wa pili," alisema Massanza.

Gadiel, amejiunga na Singida, baada ya kuachana na Chippa United ya Afrika Kusini, timu alijiunga nayo Agosti, mwaka jana.

Mchezaji huyo anayecheza nafasi ya beki wa kushoto, aliondoka nchini Januari mwaka jana, kwenda kucheza soka la kulipwa Afrika Kusini, ambapo alijiunga na klabu ya Cape Town Spurs akitokea Singida Big Stars, lakini alirejea nchini kwa muda, kabla ya kuchukuliwa na Chippa United.

Beki huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Tanzania (Taifa Stars), ni mmoja kati ya wachezaji wachache waliowahi kuzitumikia klabu kubwa nchini, Simba, Yanga na Azam.

Beki huyo alipandishwa na Azam kutoka kikosi cha vijana chini ya miaka 19 mwaka 2014, akiichezea timu hiyo hadi mwaka 2017, alipotimkia Yanga, kabla ya kuchukuliwa na Simba miaka miwili baadaye.

Katika kipindi cha dirisha dogo la usajili lililofungwa Januari 15, mwaka huu, Singida Black Stars imewasajili, Serge Pokou, raia wa Ivory Coast kutoka Al Hilal Omdurman ya Sudan, Eliuter Mpepo na golikipa Amas Obasogie, raia wa Algeria, ambaye amesajiliwa na Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili, lakini amepelekwa kwenye klabu hiyo kwa makubaliano maalum, kwa mujibu wa Masanza.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilisimama kupisha mashindano ya Kombe la Mpinduzi, Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho Afrika na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo zimepelekwa hadi Agosti, mwaka huu sasa itarejea tena kuanzia Februari Mosi.

Kikosi cha Singida Black Stars kilichokuwa kimeweka kambi jijini Arusha kimerekea mkoani Singida ili kujiandaa na mchezo dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa Februari 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Liti.



Wachezaji wa timu za programu za vijana za Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), za umri chini ya miaka 15 na 17 wakifanya mazoezi kwenye Kituo cha Mnyanjani jijini, Tanga ili kujiandaa na mashindano mbalimbali ya kimataifa. **PICHA: TFF**

# Polisi Tanzania hesabu kali

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Polisi Tanzania imekamilisha usajili wa wachezaji sita katika kipindi cha dirisha dogo la usajili wakitokea Biashara United, Singida Black Stars na Mtibwa Sugar.

Ofisa Habari wa Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi cha Championship, Frank Lukwaro, alisema usajili huo umefanywa kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi ambalo lilitaka kuongeza nguvu kuelekea mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Lukwaro aliwataja wachezaji waliotua Polisi Tanzania ni pamoja na aliyekuwa kipa wa Biashara United, David Kissu, Benson Januari na Rehani Kibungu, Rashid Kawambwa, Mwisho Mwakisunga (Singida Black Stars), na Jofrey Luseke akitokea Mtibwa Sugar.

"Kwa sasa tumedhamiria kupata pointi tatu katika kila mchezo tutakaocheza kwenye Uwanja wa Ushirika, tunahakikisha kila anayegusa hapa anatuachia pointi zote, tunasema hivyo kwa sasa tupo vizuri sana, tumekiongezea nguvu kikosi chetu katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, tuko vizuri sana sasa hivi.

Hata tutakapokwenda kucheza ugenini, wenyeji wetu wajipange kisawasawa, kwa sababu tumeimarika, tunahitaji tupate pointi ambazo zitatutimizia malengo yetu ya kurejea tena Ligi Kuu," alisema Lukwaro.

Katika msimamo wa Ligi ya Championship, Polisi Tanzania, inashika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 19, ilizozipata baada ya kucheza michezo 15, ikishinda mitano, sare nne na kupoteza sita.

Timu mbili za juu zitapanda daraja moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Bara msimu ujao wa 2025/2026.

# New City yasajili wachezaji wapya sita

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya New City FC imesema bado inamatumaini ya kubakia katika Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao licha ya kutokuwa na mwanzo mzuri katika mechi za mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa New City, Razak Salum, alisema katika kuhakikisha wanakuwa na kikosi imara ili kufikia malengo, wamefanya usajili wa wachezaji kwa kuzingatia mahitaji muhimu ya timu hiyo.

Salum alisema mapungufu makubwa yaliyokuwapo katika timu hiyo yalikuwa ni katika safu ya ushambuliaji jambo ambalo wamelizingatia katika kipindi cha dirisha dogo.

Alisema wanaamini wachezaji wapya waliowasajili watawasaidia kufanya vizuri na kuibakisha timu hiyo katika ligi hiyo ya juu Zanzibar.

"Timefanya usajili wa wachezaji sita na tumewaacha wachezaji sita, matumaini yetu ni kuhakikisha usajili huu tuliofanya utatuvusha hapa tulipo katika msimamo wa ligi," alisema meneja huyo.

Aliongeza mipango ya timu hiyo katika maandalizi ya mzunguko wa lala salama tayari imeshacheza michezo miwili ya kirafiki.

"Michezo ya kirafiki tuliyocheza itatusaidia kukijenga kikosi chetu, tayari kimeanza kupata muunganiko mzuri kati ya wachezaji wapya na wale wa zamani. Mipango yetu ni kucheza michezo minne ya kirafiki kabla ya kuanza tena kwa ligi ambayo ratiba inatarajiwa kutolewa wiki hii," meneja huyo alisema.

Katika msimamo wa ligi hiyo, New City FC ipo kwenye nafasi ya tatu kutoka mkiani ikiwa na pointi 15, imeshinda michezo minne, wametoka sare michezo mitatu na wamefungwa michezo nane. Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayofanyika kwa kuandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

HABARIMICHEZO

## ZISIKUPITE

### CUNHA ATAJWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imemfanya mshambuliaji wa Wolves na Brazil, Matheus Cunha, kuwa shabaha yao kuu ya Januari katika harakati za kufuzu mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### ARSENAL YAMTAKA CUNHA

ARSENAL pia wameonyesha nia ya kutaka kumsajili, Mtheus Cunha, ambaye ni raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 25 katika uhamisho wa Januari hii. ***(Fichajes)***
*

### GARNACHO ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanatazamiwa kufanya mazungumzo zaidi na Manchester United kuhusu winga wa Timu ya Taifa ya Argentina, Alejandro Garnacho, mwenye umri wa miaka 20, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50. ***(Telegraph)***

### UNITED YAHITAJI WINGA

MANCHESTER United imewaulizia mchezaji wa Bournemouth na Hungary, Milos Kerkez, mwenye umri wa miaka 21, nyota wa Wolves na Algeria, Rayan Ait-Nouri (23) na kiungo wa Crystal Palace, Tyrick Mitchell (25), huku kipaumbele cha Kocha, Ruben Amorim, kikiwa kumsajili winga wa kushoto. ***(The Sun)***

### NKUNKU SOKONI RASMI

CHELSEA inataka pauni milioni 70 kabla ya kumwachia mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Christopher Nkunku, mwenye miaka 27, ili kujiunga na vigogo wa Ujerumani, Bayern Munich. ***(Sky Sports)***

### ANTONY AKARIBIA BETIS

WINGA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Brazil, Antony, mwenye miaka 24, anakaribia kukamilisha uhamisho wa mkopo wa kuelekea Real Betis. ***(Sky Sports)***

### DIBLING AGEUKA LULU

TOTTENHAM Hotspur na RB Leipzig ndio klabu mbili zilizojaribu kumsajili kiungo wa kati wa Southampton, Tyler Dibling, mwenye umri wa miaka 18. ***(Sky Germany)***

### JUVE, DORTMUND VITANI

JUVENTUS na Borussia Dortmund zinawania kumsajili beki wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ureno, Renato Veiga, mwenye umri wa miaka 21, ambaye anaweza kupatikana kwa mkopo au uhamisho wa kudumu. ***(Times)***

### RASHFORD ANUKIA MARSEILLE

MARSEILLE imekuwa klabu ya hivi karibuni zaidi kuonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 27. ***(L'Equipe)***

### BARCA: KARIBU RASHFORD

BARCELONA imemtoa ofa ya kumsajili, Marcus Rashford, sehemu ambayo mchezaji huyo wa kimataifa wa England anaitaka. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH AWEKA HISTORIA

Ni nyota wa kwanza wa Liverpool kufikisha mabao 50 Ulaya...

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah amesema „najivunia sana" kuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya klabu hiyo kufunga mabao 50 katika mashindano ya Ulaya baada ya goli lake katika ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Lille.

Salah alifunga bao la kuongoza mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield Jumanne usiku huku kikosi cha Arne Slot kikijihakikishia kufuzu moja kwa moja kwa hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji aliyetokea benchi, Harvey Elliott, alihakikisha ushindi wa Liverpool katika kipindi cha pili baada ya Jonathan David kuisawazishia Lille, ambao walipunguzwa hadi wachezaji 10 baada ya Aïssa Mandi kutolewa kwa kadi ya pili ya njano iliyozaa nyekundu.

"Kwa kweli ni jambo ambalo ninajivunia sana na linakuja na ushindi kwa hiyo ni nzuri," alisema Salah akiiambia TNT Sports baada ya mchezo.

"Ni kitu cha ajabu. Kuwa mchezaji wa kwanza kufikia hilo inanifanya nijivunie sana na ni fahari kwangu."

Salah ameifungia Liverpool mabao 45 katika Ligi ya Mabingwa Ulaya (pamoja na moja katika raundi za kufuzu) na matano kwenye Ligi ya Europa.

Kwa jumla mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Misri, amefunga mabao 61 katika mashindano ya Ulaya kwa muda wote akiwa FC Basel (7), Chelsea, Fiorentina (1), Roma (3) na Liverpool.

Liverpool sasa wameshinda michezo yao yote saba katika Ligi ya Mabingwa msimu huu na pia wako pointi sita juu ya msimamo wa Ligi Kuu England.



# RAPHINHA 'AOGA' MATUSI AKIIVUSHA BARCA 16 BORA

**LISBON, Ureno**

MSHINDI wa mechi, Raphinha amesema matusi ya Benfica yalizua mzozo uwanjani baada ya bao lake la dakika za lala salama kuipa Barcelona ushindi mnono wa magoli 5-4 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa kwenye Uwanja wa da Luz, Jumanne usiku.

Bao la Raphinha dakika ya 96 lilikuwa muhimu kwa Barca katika mchezo ulioshuhudia mvua kubwa ikinyesha huko jijini Lisbon, huku vurugu kubwa zikiibuka kwa wachezaji na Raphinha akimwagiwa matusi.

"Mimi ni mtu ninayemheshimu kila mtu," alisema Raphinha, ambaye aliwahi kuwachezea wapinzani wa Benfica, Sporting CP, akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Wakati natoka uwanjani watu walikuwa wakinitukana, nikarudisha matusi, najua sitakiwi, ilinikasirisha na wachezaji wa Benfica waliendelea kunitukana.

"Mimi ni mtu ambaye ninaheshima kwa anayeniheshimu, lakini sinyamaziki wakinitusi. Ni kawaida baada ya kumalizika kwa mechi kama hiyo."

Usiku ambao haukuweza kusahaulika ulikuwa umejaa matukio ya vurugu, huku Raphinha akisema yuko katika kiwango bora zaidi cha maisha yake ya soka baada ya kufunga mabao mawili huku Barca ikishinda mara sita mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na hivyo kufuzu moja kwa moja hatua ya 16 bora.

Raphinha sasa amefikisha mabao nane kwenye michuano hiyo ya Ulaya msimu huu akiwa amepitwa tu na Robert Lewandowski aliyefunga mabao tisa na kufikisha jumla ya magoli 22 katika mashindano yote.

"Nadhani niko katika wakati bora zaidi wa uchezaji wangu, ndio," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

"Tulijua itakuwa ngumu hapa, tulijua jinsi walivyokuwa wazuri, haswa kucheza mbele ya mashabiki wao, wachezaji wao mmoja mmoja na kama timu, lakini cha muhimu ni kwamba tulijua kuweka umakini wetu wakati wote wa mchezo.

"Tulikuwa na mawazo tunaweza kubadilisha mchezo baada ya mapumziko, tukafunga bao la pili ili kurejea mchezoni na tukafanikiwa kufanya hivyo mwishoni. Hatukukata tamaa na tukaandika ushindi."

Benfica hapo awali ilitumia fursa ya makosa kadhaa ya Barca kuongoza 3-1 hadi mapumziko kwa hat trick ya Vangelis Pavlidis.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ugiriki alifunga bao la kwanza dakika ya pili na kukamilisha matatu ndani ya nusu saa baada ya Lewandowski kusawazisha kwa penalti.

"Ulikuwa mchezo wa kichaa," alisema Kocha wa Barca, Hansi Flick katika mkutano na waandishi wa habari.

"Benfica walifanya vizuri sana hasa kipindi cha kwanza, lakini tulifanya makosa mengi. Hatukulinda vizuri.

"Ni muhimu tuzungumze juu ya hili. Wapinzani wanaofuata wataangalia mechi hii na lazima tuifanye vizuri zaidi. Tutafanya hivyo.

"Wakati wa mapumziko tulisema tunataka kubadilisha kitu; tunahitaji nafasi nzuri zaidi. Na tulisema tunataka kurejea."

"Jambo bora zaidi ni mawazo ya timu katika kipindi cha pili, wanajiamini kila wakati," Flick aliongeza.

"Nilikuwa na furaha na pointi moja, lakini kwa tatu ni bora zaidi. Ilikuwa umaliziaji mzuri. Tunawekeza sana katika kipindi cha pili, tunatengeneza nafasi nyingi zaidi na tulistahili."

Ushindi huo unamaanisha Barca wamekata tiketi ya kuingia hatua ya 16 bora wakiwa na mchezo mkononi nyumbani dhidi ya Atalanta ya Italia wiki ijayo.

"Kufikia moja kwa moja hatua ya 16, hii itatusaidia sana kwa msimu uliosalia, nina uhakika asilimia 100 juu ya hilo," alisema Flick.

# Simeone: Alvarez ni mtu maalum Atletico

**MADRID, Hispania**

KOCHA Diego Simeone amesema Julián Álvarez anatarajiwa kuishia "mahali maalum" na Atlético Madrid baada ya kufunga mara mbili katika mechi iliyomalizika kwa ushindi wao wa magoli 2-1 dhidi ya Bayer Leverkusen hapo Jumanne usiku.

Atlético walikuwa wakipambana baada ya kiungo, Pablo Barrios, kutolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 25 kwenye dimba la Metropolitano, na kisha Piero Hincapié kuwaweka wageni Leverkusen mbele kwa 1-0 kabla ya kipindi ya mapumziko.

Álvarez alisawazisha na kuiweka Atlético nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa na pointi 15 kutokana na michezo saba waliyocheza.

"Tulipokuwa tukifikiria kuhusu kumsajili Julian, hili ndilo tulilofurahia," alisema Simeone akiiambia Movistar.

"Ana uzoefu wa ajabu. Ni mchezaji ambaye atakuwa na maisha bora zaidi ya baadaye.

"Tutegemee tunaweza kumsaidia kama timu, na aendelee kuwa na unyenyekevu alionao wa kuendelea kukimbia, kufanya kazi na kupigania kila kitu, kwa sababu sina shaka miaka inavyosonga, itamwacha ndani, mahali maalum katika klabu hii."

Atlético wamejivunia ushindi mkubwa katika Ligi ya Mabingwa wa msimu huu hadi sasa, wakiwafunga Paris Saint-Germain mabao 2-1 hapo Novemba na sasa wakiwazidi Leverkusen.

Watacheza dhidi ya RB Salzburg katika mchezo wao wa mwisho wa awamu ya ligi wakiwa na nafasi kubwa ya kutinga nane bora.

"Ni mchezo ambao utakumbukwa na watu waliouona," alisema Simeone.

"Walikuwa bora katika kipindi cha kwanza. Hawakuturuhusu kupata mpira. Timu moja ilicheza, na nyingine haikuingia kwenye mchezo.

"Kilichotokea kipindi cha pili sio bahati mbaya, timu imefanya hivyo katika michezo mingine. Tulisawazisha, walikuwa na kadi nyekundu, tulihisi tunaweza kushinda. Tulichukua nafasi tuliyopata na kushinda."

Álvarez alikiri mchezo huo ulikuwa wa kusisimua wa maisha yake ya Atlético hadi sasa, tangu ajiunge nayo kutoka Manchester City majira ya joto yaliyopita.

"Labda ndio, kwa kila kitu kilichotokea," alisema Álvarez akiiambia Movistar.

# Ancelotti akanusha kuondoka Madrid



**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti amekanusha taarifa za kuamua kuondoka Real Madrid msimu wa majira ya joto, akisema "Sitaamua tarehe yangu ya kuondoka katika klabu hii."

Kituo cha redio cha Hispania cha Onda Cero Jumatatu kiliripoti Ancelotti, ambaye mkataba wake utaendelea hadi mwakani, alikuwa tayari ameamua kuondoka, bila kujali kitakachotokea kati ya sasa na mwisho wa msimu.

"Hapana. Nataka kuwa wazi kabisa. Sitaamua tarehe yangu ya kuondoka katika klabu hii," alisema Ancelotti katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Salzburg hapo jana.

"Najua siku itakuja. Lakini siku hiyo itafika lini, sijui. Sitaamua. Inaweza kuwa kesho, baada ya mchezo unaofuata, mwaka mmoja au miaka mitano."

"Nina lengo. Tuna Florentino Pérez hapa kwa miaka mingine minne," aliongeza Ancelotti.

"Ananifahamu vizuri, na lengo ni kuwa hapa kwa miaka hiyo minne. Tunaweza kuondoka pamoja."

Real Madrid wako kileleni katika LaLiga, pointi mbili mbele ya Atletico Madrid na saba mbele ya Barcelona.

HABARI MICHEZO

# BOSI BODI YA LIGI AIBUKA KUIFUNDA MTIBWA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa zamani wa Bodi ya Ligi, Ahmed Yahya, amewataka viongozi wa Mtibwa Sugar wasirudie tena makosa waliyoyafanya msimu uliopita kwa kuiacha timu hiyo kushuka daraja kirahisi, iwapo itafanikiwa kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Yahya, ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa klabu hiyo na Kagera Sugar kwa nyakati tofauti alisema ilikuwa ni fedheha kubwa kwa Mtibwa Sugar kushuka daraja jambo ambalo lilikuwa ndani ya uwezo wao kuinusuru na janga hilo.

Bosi huyo alisema kushuka daraja kwa Mtibwa Sugar pia kuwe ni mfundisho kwa wachezaji nchini kujifunza kupambana kucheza kwa juhudi ili kuepuka hatari hiyo.

"Wanamichezo sasa waamke, waki-wa kwenye Ligi Kuu wasifanye masihara, wajue kupanda ni shida sana kuliko kushuka, huku kwenye ligi timu angalau zinapata fedha, kule hakuna, halafu unatakiwa upande, maana yake uvute soksi kweli kweli.

Naiombea Mtibwa Sugar ipande na nawahakikishia mashabiki wa Morogoro msimu ujao itakuwepo, na waiunge mkono. Najua itarudi kivingine Ligi Kuu kwa sababu tayari wameonja uchungu wa kushuka na kucheza madaraja ya chini, hawatarudia tena makosa yale," alisema bosi huyo.

Kuhusu tatizo lililoikumba timu hiyo iliyoshuka daraja msimu uliopita, alisema shida ilikuwa ni utawala.

"Shida ilikuwa na matatizo ya kiutawala, wakati timu inawaka kati ya mwaka 1999 na 2000 tukachukua ubingwa wa Tanzania Bara, kulikuwa na watu wa mpira pale, alikuwapo Jamal Bayser, Lawrence Gama (aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro), mimi (Yahya) kama mwenyekiti wa klabu, tulikuwa tunajua tufanye nini ili timu iwake, japo hatukuwa na pesa nyingi kihivyo, lakini tulikuwa na mikakati," aliongeza bosi huyo.

Mtibwa Sugar inaongoza katika msimamo wa Ligi ya Championship hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, ikiwa na pointi 38, ikicheza michezo 15, ikishinda mechi 12, sare mbili na kupoteza mmoja, mabao ya kufunga 25, ikiruhusu magoli sita.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Mbeya City yenye pointi 34 wakati Biashara United ya Musoma mkoani, Mara inaburuza mkia ikiwa na pointi moja mkononi.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kuanzia Februari Mosi, mwaka huu kwa timu sita kushuka dimbani kuwania pointi tatu muhimu.

# Yanga Princess yaahidi vichapo

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuanza mzunguko wa pili kwa ushindi mnono, Yanga Princess imetamba itaendelea kutoa ‚dozi' katika kila mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), watakayocheza.

Kauli hiyo imetolewa baada ya Yanga Princess kupata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Bunda Queens, katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, kiungo mshambuliaji wa Yanga Princess, Neema Kiniga, alisema wanawaomba mashabiki na wanachama wa timu hiyo kutarajia mazuri katika mzunguko wa lala salama.

Nyota huyo alisema kikosi chao sasa kimeimarika na wanaamini watapambana kusaka ushindi ili kufikia malengo yao.

"Nafanya kile ambacho kocha ananielekeza, mimi ninazingatia sana maelekezo yake ninapokuwa kwenye uwanja wa mazoezi, ninaamini tutaendelea kuwa na matokeo mazuri katika mzunguko huu wa pili," alisema Neema ambaye alifunga bao la kwanza.

Mabao mengine katika mechi hiyo yalifungwa na Eragash Tandesse, Agness Palangyo na Asha Ramadhan.

Mechi nyingine iliyochezwa juzi, JKT Queens ilipata ushindi wa mabao 4-0 wakati Ceasiaa Queens iligawana pointi na Fountain Princess baada ya kutoka sare ya bao 1-1.



Kiungo mpya wa kimataifa wa Yanga Princess kutoka Ethiopia, Aragesh Tandesse (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Bunda Queens, Sarah Lucas, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Yanga Princess ilipata ushindi wa mabao 4-1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba: Kucheza bila mashabiki ilituumiza

INATOKA UK. 24

Hatua inayokuja ya robo fainali nadhani mechi itakuwa bora zaidi kwa sababu tutaongeza umakini sana, mashabiki wetu tunawaomba wakamilishe ile pesa wanayochanga ili waweze kuingia katika mchezo wa robo fainali na watushangilie kwa nguvu, ila wajitahidi kutorudia kilichopita," Balua alisema.

CAF pia iliwapiga faini ya Dola za Marekani 60,000 Waarabu hao wa Tunisia kufuatia wachezaji, mashabiki na viongozi wao wa benchi la ufundi kufanya vurugu katika mechi hiyo.

Ikicheza bila mashabiki, Simba ilipata ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa Kibu Denis na Leonel Ateba.

Simba sasa inasubiri kufahamu mpinzani wake wa hatua ya robo fainali kupitia droo itakayochezwa mwishoni mwa mwezi huu.

## Yanga hasira zote Ligi Kuu Bara, FA

INATOKA UK. 24

la mingi katika mitandao ya kijamii, televisheni na vipindi vya michezo, ikiwamo matamko ya baadhi ya watu wa mpira kujibu alichosema, lakini wengi wamekuwa wakijibu kitu ambacho walikuwa hawajaelewa alichokimaanisha kocha huyo.

Alifafanua Ramovis hakusema Ligi ya Tanzania ni dhaifu, kama wengi walivyoelewa na ‚kukazia hapo', badala yake alimaanisha uharaka wa matukio uwanjani katika mechi za ligi hiyo.

"Nadhani neno, ‚intensity', ndiyo limewachanganya watu, ukilitafsiri huwezi kupata neno udhaifu, badala yake ni ukali, kasi na uharaka na matukio na ndicho alichomaanisha. Mpira una matukio mawili, timu inapokuwa na mpira na inapokuwa haina, sasa ni vipi timu inajibu kwa vitendo inapokuwa naona mpira na ambapo haina mpira kwa uharaka.

Hiki ndicho alichosema kocha wetu na hata kwenye ligi mbalimbali Ulaya, Ligi ya England ina uharaka wa matukio uwanjani na kasi, kuliko ya Ufaransa, lakini huwezi kusema ni dhaifu," alisema Kamwe.

Aliongeza ubora wa ligi na uharaka wa matukio katika ligi husika ni vitu viwili tofauti, hivyo baadhi ya wadau wakiwamo wachambuzi waache kumshutumu kocha wao kwa sababu alichokisema ni sahihi na wao ndiyo wanaopotosha.

"Tunapaswa kuwa wakweli kuhusu Ligi ya hapa Tanzania, ugumu unaokutana nao unapocheza dhidi ya timu nyingine za Tanzania sio wa kiwango kikubwa sana. Ukiona Ligi za Algeria, Afrika Kusini, Morocco, Tunisia, tunahitaji nguvu na kasi hiyo ya juu ili kushindana na tuzoee hali hiyo.

Ukali na kasi ya ligi ya Tanzania, ni mdogo sana ukilinganisha na nchi hizo, wao ligi yao ni ngumu na kila timu kali sana, tunahitaji ugumu kama wa ligi hizo ili tushindane," aliongeza.

Alisema pia siku hazifanani na viwango vya wachezaji hubadilika.

"Niwaambie tu Wanayanga wote watulie, tulikuwa na siku mbaya kazini, hatukucheza kwa kiwango chetu kwa asilimia 100, nilizungumza na wachezaji wote baada ya ile mechi na niliwaambia laiti tungerudia kucheza asilimia 60 tu ya kiwango tulichoonyesha dhidi ya Al Hilal Omdurman kule Mauritania, MC Alger ilikuwa inakufa kwa Mkapa, lakini ndiyo mpira, watu wanaweza kuamka vizuri leo, kesho wakaamka vibaya," aliongeza.

# Michezo

Alhamisi Januari 23, 2025

Nipashe


**Salah aweka historia** UKURASA 21





Rais wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Wallace Karia (katikati), akiwa katika Mkutano Mkuu wa baraza hilo uliofanyika kwenye Hoteli ya Imperial Plaza jijini Juba, Sudan Kusini jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Wanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Sarah Mukuna na Makamu wa Tatu wa Rais wa shirikisho hilo, Souleiman Waberi. **PICHA: CECAFA**

# Simba: Kucheza bila mashabiki ilituumiza

## ●●●Nyota wafunguka ‘vibe’ lao huongeza kasi, nguvu, walitaja deni CAF…

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA ndio timu pekee iliyobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutoka Afrika Mashariki na Kati, wachezaji wa Simba wamesema walikutana na wakati mgumu kucheza mechi kwa mara ya kwanza wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani bila ya mashabiki.

Simba iliwakaribisha CS Constantine kutoka Algeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ikiwa bila ya mashabiki, ingawa mechi hiyo ilimalizika kwa wenyeji kupata ushindi wa mabao 2-0 na kuifanya ifikishe pointi 13 ambazo ziliwapelekea kuongoza Kundi A katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

CAF iliwaadhibu Simba kucheza bila mashabiki na kulipa faini ya Dola za Marekani 40,000 kufuatia vurugu za mashabiki zilizojitokeza katika mechi ya hatua ya makundi dhidi ya CS Sfaxien kutoka Tunisia iliyochezwa Desemba 15, mwaka jana.

Wakizungumza na gazeti hili jana, wachezaji wa Simba walisema iliwaweka katika nafasi ngumu kwa sababu hawajazoea kucheza bila mashabiki wakiwa nyumbani.

Shomari Kapombe, Edwin Balua na Yusuph Kagoma, walisema mwanzoni mwa mchezo iliwaathiri kwa kiasi kikubwa kwa sababu siku zote hucheza huku wakishangiliwa, kutiwa moyo na kuhimizwa, lakini siku hiyo kila wanapogusa mpira hawakuwa wakisikia chochote.

Kapombe alisema hali hiyo ‚iliwaumiza‘, lakini kadri muda ulivyozidi kwenda walikumbuka nini wanatakiwa kufanya katika mchezo huo.

“Mechi ile uwanjani ilikuwa nzuri sana, jamaa walizuia sana, mwanzo tulipata shida, tukatengeneza nafasi chache tukashindwa kuzitumia, kipindi cha pili mwalimu alituambia udhaifu wao na jinsi ya kuvunja ukuta wao.

Lakini kwa upande wa pili ‚hatukuinjoi‘ kucheza bila mashabiki, binafsi nainjoi tunapocheza zaidi tukiwa kando na mashabiki wetu, walihitajika sana siku ile, lakini hatuwezi kulalamika ni kitu ambacho kimetokea, tunaamini mechi ijayo tutakuwa wote na sisi tutakuwa na furaha sana, na kwa sababu hawakuwapo mechi iliyopita, mechi ya robo fainali watajaza uwanja, watashangilia sana, na watatupa moyo sana wa kupambana kwa sababu tuliwamisi mechi iliyopita, nao walitumisi pia,“ alisema Kapombe.

Kwa upande wa Kagoma alisema kwake pia lilikuwa jambo gumu, lakini baadaye alikumbuka mashabiki wao wapo sehemu fulani wamekusanyika pamoja kwa ajili ya kuwashangilia.

“Mechi ilikuwa ngumu sana, jua kali mno, pia kucheza bila mashabiki ilikuwa ngumu, ila nilikuwa nikicheza nawakumbuka, najua wapo sehemu wamekusanyana wanaangalia mpira, wanatushangilia, wengine vibanda umiza, nikivuta picha yao jinsi watakavyokuwa wanashangilia basi inanipa nguvu ya kupambana uwanjani,“ alisema Kagoma.

Winga Balua amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kumalizia deni katika ule mpango wa ‚tunawajibika pamoja‘, ili mechi ya robo fainali wajumuike pamoja uwanjani.

“Ilikuwa ngumu kucheza hivi, kwa sababu mashabiki wa Simba lile vibe lao huwa wanatuongezea kitu kikubwa sana, watuongezea umakini, kasi, nguvu na kupambana zaidi hata maeneo ambayo unaona ni magumu, lakini hatukuwa na jinsi.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga hasira zote Ligi Kuu Bara, FA CUP

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi cha Yanga kimeingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Copco FC utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Yanga iliiaga michuano ya kimataifa baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye Kundi A nyuma ya vinara Al Hilal ya Sudan, MC Alger ya Algeria huku TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), ikiburuza mkia.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walihitaji ushindi wa aina yoyote katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi, lakini matokeo ya sare ya bila kufungana yaliwafaidisha MC Alger ambayo ilifikisha pointi tisa na Yanga kufikisha pointi nane, Al Hilal alimaliza kileleni akiwa na pointi 10.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema baada ya kukosa bahati ya kutinga hatua ya robo fainali, akili na nguvu zao sasa wamezielekeza kwenye mchezo wa Kombe la FA pamoja na mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa Februari Mosi, mwaka huu.

“Timu kwa sasa imerejea kambini baada ya mapumziko ya muda mfupi, tuna mechi ya Kombe la FA dhidi ya Copco, ni mechi muhimu kwa ajili ya kurejesha nyuso za furaha kwa mashabiki wetu, tunawaahidi tutarudi kwa nguvu kubwa.

Tutahakikisha tunarudi kutetea makombe yetu yote, kuanzia hili la FA, hadi Ligi Kuu, hatuwezi kushindwa kutinga robo fainali ya Afrika, halafu pia tukapoteza makombe yetu, haya ndiyo yatatupoza machungu, na wataturudisha katika michuano kama hiyo msimu ujao,“ alisema Kamwe.

Wakati huo huo, Yanga imesema kauli iliyotolewa na Kocha Mkuu wa timu yao, Sead Ramovic, kuhusu ubora wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kutupwa nje katika michuano ya CAF, haikueleweka vyema kwa wadau.

Kamwe alisema kumekuwa na mijada-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042